epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumamosi Novemba 30, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • Na. 0581876
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

# Kilichomnasua 'RC' Nawanda kesi ya ulawiti

• **Vilio**, shangwe vyasikika mahakamani, mwenyewe asema anamwachia Mungu... *Endelea ukurasa 2*



Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahaya Nawanda (katikati), akitoka katika Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki Mahakama ya Hakimu Mfawidhi Mkoa wa Mwanza, baada ya kuachiwa huru. **PICHA: VITUS AUDAX**

UKURASA WA 22

**RODRI ADOKEZA SIKU YA KURUDI DIMBANI**



UKURASA WA 3

**Wamiliki** jengo lililoporomoka, kuua Kariakoo wapandishwa kizimbani



UKURASA WA 4

**Makalla** atambia mambo manne yaliyoibeba CCM Uchaguzi Serikali za Mitaa



UKURASA WA 4

**Aeleza** mshtakiwa kesi dawa kulevya alivyokamatwa akiwa chini ya uvungu wa kitanda



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza katika Mjadala wa Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kwenye maadhimisho ya miaka 25 ya jumuiya hiyo, jijini Arusha jana. Wengine ni Rais wa Kenya, William Rutto (kulia), Rais wa Uganda, Yoweri Museveni (wa pili kulia) na Rais wa Somalia, Hassan Sheikh Mohamud. **PICHA: IKULU**

## Wakuu nchi za EAC wakutana Arusha kwa ajenda nyeti

UKURASA 3

# Hatifungani kukusanya bil. 150/- kulipa makandarasi wa barabara

• **Rais** Samia aongoza ununuzi, Mpango... *Endelea ukurasa 5*

**MICHEZO** AHOUA AFICHUA SIRI YA PENALTI SIMBA UK.24 **KATUNI** UK.6

# Kilichomnasua Nawanda kesi ya ulawiti, mwenyewe asema anamwachia Mungu

**Na Vitus Audax,** MWANZA

"MUNGU ni mwema na kila kitu kinatoka kwa Mungu. Utukufu ni wake Mungu, yote ninamwachi Mungu." Hiyo ni kauli ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahaya Nawanda nje ya mahakama, muda mfupi baada ya kuachiliwa huru jana katika kesi ya mashtaka ya kulawiti mwanafunzi wa chuo kikuu.

Dk. Nawanda alikuwa anakabiliwa na kesi ya jinai namba 1883 ya mwaka 2024 katika Mahakama ya Hakimu Mfawidhi Mkoa wa Mwanza.

Akisoma hukumu hiyo jana Hakimu Mfawidhi Mkuu, Erick Marley alisema mahakama hiyo ilipokea mashahidi 10 na vielelezo vitatu kutoka upande wa Jamhuri pamoja na shahidi mmoja kutoka upande wa utetezi ambaye ndiye alikuwa mshtakiwa katika kesi hiyo.

Hakimu huyo alisema kuwa kati ya mashahidi wa upande wa Jamhuri, mama mzazi wa binti aliyedaiwa kuingiliwa kinyume cha maumbile, alikuwa shahidi namba moja, shahidi namba mbili ni binti mwenyewe. Wengine ni askari wa upelelezi, uchunguzi, daktari kutoka Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mwanza (Sekou Toure) na mtaalamu wa Tehama kutoka Jengo la Rock City Mall.

Alisema vielelezo vilivyowasilisishwa mahakamani huko ni pamoja na picha mjongeo (CCTV footage) za eneo la jengo hilo, gari ambako tukio lilidaiwa kutokea, vipimo vya daktari pamoja na maelezo ya awali aliyoandikisha binti huyo.

Hakimu Marley alisema mahakama ilimkuta Dk. Nawanda na kesi ya kujibu, hivyo kumpa nafasi ya kujitetea na baada ya kujiridhisha kutokana na ushahidi uliotolewa na pande zote mbili, hakutiwa hatiani.

Alitaja mambo yaliyotia shaka katika vielelezo na ushahidi uliotolewa na mashahidi hao ni pamoja na kukosekana baadhi ya vipande vya video (CCTV footage) zinazoonesha binti huyo akifanyiwa ukatili kati ya vilivyowasilishwa mahakamani.

Alisema video hizo zinamwonesha binti huyo wakati akiingia katika geti akiwa amepakizwa kwenye pikipiki, akaanza kufanya mawasiliano kisha nyingine zilionesha wakati mshtakiwa Dk. Nawanda aliposhuka kulipia ushuru wa maegesho.

Hakimu huyo alisema hakuna video zilizomwonesha binti huyo akiingia katika gari na chochote kilichoendelea ndani ya gari hilo, hivyo kutothibitisha juu ya kutendeka ukatili huo.



Baba mzazi wa aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahaya Nawanda (katikati), akilia baada ya hukumu dhidi ya mtoto wake kutolewa ikimwachia huru katika kesi ya jinai namba 1883/2024. **PICHA: VITUS AUDAX**

Vilevile, hakimu huyo alisema mahakama haikupokea ushahidi wa vinasaba (DNA) unaonesha kuwa aliyemwingilia kinyume cha maumbile ni nani licha ya binti huyo pamoja na mshtakiwa kuchukuliwa vipimo hivyo, hali iliyofanya mahakama hiyo kukosa ushahidi wa kitaalamu juu ya tukio hilo.

Hakimu Marley alisema licha ya daktari kuthibitisha kuwa binti hiyo aliingiliwa kinyume cha maumbile kutokana na sehemu zake za siri kuwa na michubuko kwa ndani na nje, ushahidi huo haukubainisha nani aliyemwingilia.

"Katika ushahidi uliotolewa na Daktari Patrick Daudi kutoka Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mwanza (Sekou Toure), alisema binti huyo alifikishwa hospitalini huko kwa ajili ya vipimo baada ya saa zaidi ya 19 tangu alipotendwa tukio hilo huku akiwa tayari ameoga na kuondoa ushahidi wa mbegu za kiume, hivyo kukosa ushahidi wa mbegu ili kudhihirisha kuingiliwa kingono na mtu yupi," alisema Hakimu Marley.

Alisema kuchelewa kwa binti huyo kwenda hospitalini huku kukiwa na mtu mwingine aliyetajwa kuwa mwenzake waliokuwa wakiishi wote, viliweka shaka juu ya kama kuna mtu mwingine aliyemtenda tukio hilo kwa muda wote huo.

"Katika ushahidi wake, shahidi namba moja ambaye ni binti huyo alieleza kuwa baada ya kutendwa tukio hilo, alikwenda moja kwa moja alikokuwa anaishi na kisha kumweleza rafiki yake kisha kuwasiliana na mama yake, lakini shahidi huyo hakumleta mahakamani hapa, pengine angekuwa shahidi muhimu," alisema Hakimu Marley.

Alisema sehemu nyingine iliyoacha shaka ni maelezo ya binti huyo aliyedaiwa kulawitiwa, kwamba alifanyiwa ukatili huo katika gari jeupe, lakini rangi yake halisi ni ya fedha.

Pia alisema binti huyo alidai kuwa wakati anafanyiwa kitendo hicho, gari lilikuwa na vioo 'tinted' na nje hakukuwa na watu waliokuwa wanapita, lakini video zilionesha gari hilo halikuwa 'tinted' na pia watu waliokuwa wakipita nje na kuendelea na shughuli zao.

Alisema kuwa baada ya Dk. Nawanda kukutwa na kesi ya kujibu, alipotakiwa kujitetea, alikiri kuwa siku hiyo ya tukio alifika katika eneo hilo kwa ajili ya kuchukua mahitaji yake na pia alikiri kuwasiliana na binti huyo kama rafiki yake na hawakutumia muda mrefu aliondoka kwa kuwa alikuwa na miadi na watu wengine.

Hakimu huyo alisema kama ilivyo kwa mujibu wa video za CCTV, aliingia eneo hilo saa 2:48 na kutoka saa 3:11 usiku, wakitumia dakika 23 pekee na kuwa yeye na binti huyo hawakuwahi kukutana katika gari na wala gari hilo halikuwa na vioo vyeusi (tinted) kama alivyodai binti huyo.

Baada ya kusikiliza pande zote, Hakimu Marley alimwachilia huru Dk. Nawanda na kueleza kuwa kutokana na kasoro hizo zilizojitokeza na baada ya kuhusianisha na kesi nyingine za namna hiyo, mahakama haikumkuta na hatia mshtakiwa huyo, hivyo yuko huru.

Baada ya kutolewa kwa hukumu hiyo katika mahakama hiyo iliyokuwa imefurika watu, Nipashe ilishuhudia hisia tofauti vilio na kelele za shangwe.

Katika ufuatiliaji wake, mwandishi alibaini binti huyo aliyedai kutendwa ukatili huo, pia mama yake mzazi hawakuwapo wakati hukumu hiyo ikisomwa.

Akizungumza nje ya mahakama hiyo, Dk. Nawanda alisema anamshukuru Mungu kwa kila kitu pamoja na ndugu, jamaa na marafiki na mawakili waliosimama naye katika kipindi hicho chote.

"Ninaishukuru familia yangu, ninaishukuru mahakama imetenda haki, Wakili Alex kwa kazi kubwa aliyofanya, ninamshukuru Mungu kwa kila kitu. Mungu ni mwema na kila kitu kinatoka kwa Mungu na utukufu ni wake Mungu. Asenteni sana! Ninamwachia Mungu," alisema Dk. Nawanda.

Wakizungumza nje ya Kituo Jumuishi katika Mahakama ya Hakimu Mfawidhi Mkoa wa Mwanza, mawakili wa upande wa utetezi, wakiongozwa na Costantine Mutalemwa, walisema mteja wao hana nia ya kufungua shauri la kuchafuliwa kisiasa kwa kuwa kila kitu mteja wao amemwachia Mungu.

Dk. Nawanda alipandishwa kizimbani kwa kwa mara ya kwanza Julai 9, 2024 na kusomewa shtaka moja la kumlawiti binti huyo, kitendo ambacho ni kinyume cha kifungu namba 154(1)(a) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, SURA 16.

Alidaiwa kutenda tukio hilo Juni 2 mwaka huu, akidaiwa kumtenda ukatili huo mwanafunzi huyo wa chuo kikuu cha mkoani Mwanza katika eneo la maegesho ya magari lililoko Rock City Mall, wilayani Ilemela, mkoani Mwanza.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***




# Vilio vyatawala mwili wa Dk. Ndugulile ukiwasili

**Na Restuta James**

VILIO, simanzi vyatawala jana wakati mwili wa Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika, Dk. Faustine Ndugulile, ulipowasili Uwanja wa Ndege wa Kimataifa, Julius Nyerere (JNIA).

Dk. Ndugulile alifariki dunia Jumatano wiki hii wakati akipatiwa matibabu nchini India.

Naibu Spika wa Bunge, Musa Azan Zungu, aliongoza viongozi mbalimbali waliojitokeza uwanjani hapo kuupokea mwili huo.

Viongozi wengine waliojitokeza ni mawaziri, wabunge, wakuu wa wilaya na watumishi wa Ofisi ya Bunge ambao waliungana na familia ya marehemu, kuupokea mwili huo, ambao ulipelekwa moja kwa moja Hospitali Kuu ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Lugalo.

Akizungumza na waandishi wa habari uwanjani hapo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, alimwelezea Dk. Ndugulile kama kiongozi aliyesimamia kile alichokiamini, hasa kikiwa kina maslahi ya wengi.

"Kama nchi tumepoteza mtu muhimu katika wakati muhimu. Alikuwa mtaaluma mzalendo, asiyebabaika na mazingira na mawimbi. "Nafasi ambayo aliipata WHO ilikuwa inakwenda kutusaidia na kunufaika kwa kuzaliwa kwake Tanzania. Ni huzuni kubwa," alisema.

Simbachawene alisema alimfahamu Dk. Ndugulile tangu mwaka 2010 alipochaguliwa kwa mara ya kwanza na wananchi wa Kigamboni kuwa mbunge.

Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee, alisema Dk. Ndugulile alikuwa ni mbunge wa aina yake, aliyetetea maslahi ya wananchi bila kujali itikadi za vyama.

Alisema ni kiongozi ambaye alikuwa mwerevu asiye na majivuno, ambaye aliwahi kushika shilingi bungeni, kutetea maslahi ya wananchi.

"Aliaminiwa na taifa, akasogezwa mbele kuwania nafasi hiyo ya kimataifa. Kwa hakika, nchi imepata pigo kubwa kwa kifo chake," alisema.

Baadhi ya viongozi walioambatana na familia kuupokea mwili huo, ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), William Lukuvi, wabunge wa Dar es Salaam, wakuu wa wilaya za Kigamboni na Temeke na baadhi ya wakazi wa jimbo la Kigamboni.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa juzi na Ofisi ya Bunge, kesho kutwa (Jumatatu) mwili utatolewa Lugalo na kupelekwa Parokia ya Mtakatifu Immaculata, Upanga, Dar es Salaam, kwa ajili ya ibada na kisha utapelekwa viwanja vya Karimjee kwa ajili ya mazishi ya kitaifa, yatakayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Baada ya Karimjee, mwili utalala nyumbani kwake Kigamboni na kesho yake, utapelekwa viwanja vya Machava, Kigamboni kwa ajili ya wananchi wake kumuaga na baadaye utazikwa katika makaburi ya Mwongozo, yaliyoko Kata ya Mwongozo, wilayani Kigamboni.

Dk. Ndugulile aliyezaliwa Machi 31, 1969, alifariki dunia Novemba 27, mwaka huu, akiwa nchini India alikokwenda kutibiwa.

# Wakuu EAC wakutana kwa ajenda nyeti

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WAKUU wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) jana walikutana jijini hapa kujadiliana mambo mbalimbali muhimu kuhusu ushirikiano na maendeleo baina yao.

Miongoni mwa mambo waliyojadiliana ni kuondoa vikwazo visivyo vya kikodi, uzalishaji wa bidhaa na masoko ya bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi wanachama na masuala ya ulinzi na usalama.

Viongozi hao walikutana pia katika maadhimisho ya miaka 25 ya EAC ambayo ilianishwa mwaka 1999. Kabla ya kuanzishwa, jumuiya hiyo ilikuwapo kuanzia mwaka 1967 kabla ya kuvunjika mwaka 1977.

Rais Samia Hassan Suluhu alizitaka nchi za EAC kuunga mkono jitihada za matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kuwezesha wanawake kutopata madhara kiafya sambamba na vijana kupata ajira husasan wa vijijini kwa kupata umeme wa uhakika.

Pia alisema mabadiliko ya tabianchi yana athari kubwa katika nchi, hivyo Tanzania imejipanga kuhakikisha matumizi ya nishati safi yanakuwa kwa kasi katika maeneo ya vijijini na mijini.

Alisema Tanzania inajitahidi kupambania matumizi ya nishati safi ya kupikia na inahitaji zaidi ya dola milioni 19 katika kipindi cha miaka mitano kwa ajili ya kurekebisha masuala la mazingira, hivyo kila wilaya nchini Tanzania iendelee kupanda miti ingawa kasi yake ni ndogo.

"Tanzania imejipanga kuhakikisha matumizi ya nishati safi ya kupikia yanakua ikiwamo kupunguza wimbi la vijana kukimbia mjini kwani hivi sasa wanapata ajira huko vijijini na kinamama kutumia nishati ya umeme."

Alisema wanawake wanapata matatizo mbalimbali kutokana na matumizi ya kuni hivyo lazima kuhakikisha wanawake wanaondoka na matumizi ya nishati hiyo nawaomba wakuu wa nchi waniunge mkono kuhakikisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Tanzania, alisema imekuja na sera ya upandaji miti kila mwaka kwa kila wilaya lakini bado kasi haijakuwa nzuri.

Katika mapambano ya nishati chafu Tanzania inapambana si kuhakikisha inasambaza umeme vijijini ili kuwezesha wanawake kupikia, ikiwamo vijana kujiajiri ikiwamo kusambaza umeme wa gesi, kwani nusu ya umeme wa Tanzania unatokana na maji ikiwamo mabwawa ya maji.

Alisema katika suala la mabadiliko ya tabianchi, lazima kila nchi ya EAC kukubaliana kwa pamoja ili kuunganisha nguvu na kusisitiza nchi hizo kushirikiana na sekta binafsi ili kuwezesha matumizi ya nishati hivyo yanakuwa kwa kasi.

Alisema ukosefu wa ajira na nyenzo za vijana kujipatia ajira hivyo Tanzania imekuja na mpango wa BBT kwa kuhakikikisha vijana wanajiajiri katika kilimo na mipango mingine ya kisera ikiwamo kilimo, mifugo na misitu hivyo Tanzania imetengeneza uwanda mpana kwa vijana ili wajue kilimo ni ajira.

Alisema tatizo kubwa la vijana ni kupata ardhi, fedha, teknolojia hivyo serikali ya Tanzania imetenga maeneo makubwa mfano Dodoma kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji ikiwamo utoaji wa ardhi na hati ikiwamo kujengewa makazi na kuunganishwa katika mnyororo wa soko ikiwamo uunganishaji wa vijana na benki ili kutoa mikopo kwa vijana kwa ajili ya kilimo.

Rais wa Somalia, Hassan Sheikh Mohamud, alisema ni vyema kuongeza uwezekano wa mazao ya kilimo, uvuvi, viwanda na mifugo, kufikia masoko mapana kwani sekta hizo ni muhimu kwa uchunguzi lakini pia miradi ya kikanda katika uchukuzi na uunganishaji wa nishati katika kuipatia Somalia fursa ya kuimarisha miundombinu na kuunganisha masoko.

Huku Rais William Ruto wa Kenya alisisitiza umuhimu wa amani na utulivu katika pembe za Afrika ikiwamo nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kuisaidia zaidi nchi ya Congo katika masuala ya amani.

Alisisitiza kipaumbele zaidi katika kuimarisha mikataba ya biashara kwa kuanzisha mikataba mipya inayoimarisha kilimo na miundombinu ikiwamo kusaidia wafanyabiashara wa viwanda vidogo na vya kati na utoaji mafunzo na rasilimali kwa wawezekaji haswa maeneo ya mipakani.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations @guardian.co.tz***




Mwenyekiti wa Bodi wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Stephen Wasira, akihutubia katika mahafali ya 19 ya wahitimu wa chuo hicho, Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Harun Mapesa na (katikati) ni Naibu Mkuu wa Chuo anayesimamia Taaluma, Utafiti na Ushauri Kitaalamu, Prof. Richard Kangalawe. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wamiliki jengo lililoporomoka Kariakoo wafikishwa kizimbani

**Na Grace Gurisha**

WANAODAIWA kuwa wamiliki wa jengo la ghorofa Kariakoo ambalo liliporomoka na kusababisha vifo vya watu 31, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kwa tuhuma za kuua bila kukusudia.

Washtakiwa waliofikishwa mahakamani hapo ni Leon Mdete (49) mkazi wa Mbezi Beach, Zenabu Islam (61) mkazi wa Kariakoo na Ashour Ashour (38) mkazi wa Ilala na wote ni wafanyabiashara.

Wakisoma hati ya mashtaka jopo la mawakili watatu wa serikali , Adolf Lema, Grace Mwanga na Eric Kamala mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Godfrey Mhini, ilidaiwa kuwa washtakiwa hao wanatuhumiwa kwa mashtaka 31.

Ilidaiwa kuwa washtakiwa hao, Novemba 16, 2024 katika Mtaa wa Mchikichi na Congo, Kariakoo jijini Dar es Salaam, isivyo halali, kwa pamoja walishindwa kutimiza majukumu na kusababisha vifo vya watu 31.

Watu hao waliofariki ni Said Juma, Hussein Njou, Prosper Mwasanjobe, Shadrack Mshingo, Godfrey Sanga, Neema Sanga, Elizabeth Mbaruku, Hilary Minja, Abdul Sululu na Chatherine Mbilinyi.

Wengine ni Elton Ndyamkama, Mariam Kapekekepe, Elizabeth Kapekele, Hadija Simba, Frank Maziku, Rashid Yusuf, Ally Omary, Ajuae Iyambilo, Mary Lema, Khatolo Juma, Sabas Swai, Pascal Ndungulu, Brigette Mbembele, Ashery Sanga, Venance Aman, Linus Hasara, Issa Bakari, Lulu Sanga, Happnees Mallya na Brown Kabovera.

Baada ya kuwasomea mashtaka hayo, Hakimu Mhini aliwaeleza washtakiwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi yao, hivyo hawatakiwi kujibu chochote.

Upande wa mashtaka ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika, hivyo kuiomba mahakama ipange tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Mhini alisema ili washtakiwa wawe nje kwa dhamana, wanatakiwa kuwa na wadhamini wawili kila mmoja wenye barua za utambulisho, kitambulisho cha taifa na watatakiwa kutia saini bondi ya Sh. milioni tano kila mmoja.

Mshtakiwa Mdete alitimiza masharti na kuachiwa kwa dhamana lakini Islam na Ashour walipelekwa mahabusu baada ya kushindwa kutimiza masharti hayo.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Desemba 12, mwaka huu, kwa kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi ilipofikia.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations @guardian.co.tz***

# CCM yataja sababu nne ushindi Serikali za Mitaa

**Na Romana Mallya**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimetaja sababu nne za ushindi wa kishindo katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kuwakosoa wanaoainisha matukio ya mauaji na waliojeruhiwa katika uchaguzi huo kwa kuegamea vyama vya upinzani pekee.

Kimetaja matukio sita ya makada wake miongoni akiwamo aliyeuawa kwa risasi na kusisitiza kwamba, wanapokemea na kueleza kasoro zielekezwe kwa vyama vyote.

Kadhalika, kimewataka watu kuondokana na dhana potofu kwamba, CCM kikishindwa katika uchaguzi ndio demokrasia ya kweli.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Amos Makalla, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uchaguzi huo uliofanyika Jumatano nchini.

Makalla alisema imani iliyooneshwa na Watanzania kwa CCM inatokana na mambo mbalimbali ikiwamo watu kuridhika na utekelezaji mzuri wa ilani kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo na utatuzi wa kero.

Sababu ya pili aliitaja ni maandalizi ya uchaguzi yaliyofanywa na CCM kujiandaa vizuri kwa kufanya tathmini ya viongozi walioko katika mitaa, vijiji na vitongoji.

"Chama Cha Mapinduzi hakikukosea kuteua wagombea safi ambao wanakubalika, hiyo ndio siri ya ushindi. Sitarajii mtu akaja akahoji CCM imeshindaje. Ninyi ni mashahidi vyama vingine havikuwa na maandalizi ya kutosha, havijaonekana kwa wananchi zaidi ya miezi saba zaidi ya maandamano.

"Unakwenda kwenye uchaguzi kwa siku tatu unamwona mwenyekiti wa taifa anakwenda Ipinda, Songwe, Mbeya na kuamini kwamba, uchaguzi umefanyika na hataweza kushinda. Itakuwa ni maajabu na kichekesho," alisema.

Alisisitiza changamoto ambayo upinzani imeipata ni kwamba hawakujiandaa na maandalizi ya uchaguzi.

Makalla ambaye ni Mlezi wa Mkoa wa Dar es Salaam alisema, Dar es Salaam wameshinda mitaa 563 na kupoteza mtaa mmoja wa Tandika baada ya Chama cha ACT-Wazalendo kushinda.

Alitaja sababu ya tatu ya ushindi CCM kuwa umechangiwa na utaratibu wa kampeni ambazo wamezifanya kisayansi kuanzia uzinduzi hadi kuzifunga.

"Sababu ya nne, ni wazi kwamba migogoro ndani ya vyama vya siasa imeipa nafasi CCM kushinda uchaguzi huu, wapinzani wanapitia wakati mgumu wana migogoro ndani.

"Huwezi ukapata ushindi kwa matukio yaliyotokea Arusha, wiki hiyo mnagombana, mnapigana, mnarushiana makonde halafu ushinde katika mkoa wa Arusha, ni jambo haliwezekani.

"Mmeshuhudia viongozi wao wa kitaifa wamegawanyika mmoja anasema hiki, mwingine anasema hiki, mmoja kajiandikisha, mmoja hajajiandikisha, inaonesha safari hii hawajajipanga," alisema.

Kutokana na hilo, Makalla alishauri waendelee kuvijenga vyama, kuvumiliana, kutengeneza umoja kwa sababu hawawezi kujenga chama kama kuna mgogoro au hawapo pamoja.

Kiongozi huyo aliwataka watu kuondokana na dhana potofu kwamba, CCM kikishindwa katika uchaguzi ndio demokrasia ya kweli.

"CCM kinachaguliwa na wananchi hakijiweki chenyewe madarakani, ikionekana pale CCM inapoteza kwa wingi basi ndio demokrasia, lakini ikishinda sio demokrasia. Mnaeleza kasoro mbalimbali nyingi kupotosha. CCM inabebwa na kazi nzuri zinazofanywa na serikali," alisema.

Makalla alisema wanaosubiri demokrasia ya kweli ni pale CCM itakapoanguka, haitatokea kwa sababu watahakikisha wanakonga nyoyo za Watanzania ili kuendelea kuaminika.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations @guardian.co.tz*



Balozi wa Tanzania nchini Comoro, Said Yakub (wa tatu kushoto), akiwapokea madaktari 20 kutoka hospitali mbalimbali Tanzania waliowasili nchini humo jana, kwa ajili ya kutoa matibabu ya kibingwa kwa wagonjwa mbalimbali. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Shahidi aeleza mshtakiwa dawa kulevya alivyokamatwa chini ya uvungu wa kitanda

**Na Kulwa Mzee**

KOPLO Gladness ameieleza mahakama walivyomkamata mtuhumiwa wa dawa za kulevya kwenye uvungu wa kitanda na wengine wawili ndani ya basi la Tashrif, kituo cha Mbezi, wakisafiri kwenda Tanga.

Gladness, ambaye ni shahidi wa upande wa Jamhuri, alidai hayo jana katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Godfrey Isaya, akiongozwa na Wakili wa Serikali, Sabina Ndunguru.

Shahidi alidai walimkamata mshtakiwa wa kwanza, Maliki Jafari Maliki, chini ya uvungu wa kitanda, nyumbani kwake na wengine, Ally Maliki na Iddi Nassoro ndani ya basi kisha wakawashusha.

Akitoa ushahidi huo, alidai kuwa Machi 22, 2022 akiwa nyumbani, alifahamishwa na Afande Hassan kuwa kuna mtu anajihusisha na biashara ya dawa za kulevya maeneo ya Temeke.

Alidai kuwa akiwa na askari wengine, walikwenda nyumbani kwa Maliki na walipofika Afande Lazaro aligonga mlango akatoka Delinda Salum akajitambulisha kuwa ni mke wa Maliki.

"Tulipomwulizia Maliki alisema hayupo na kwamba alikuwa anatoka alfajiri kisha tulimwambia tunataka kufanya upekuzi. Afande Hassan na Anna walimfuata mjumbe anayeitwa Tabu.

"Walipofika na mjumbe, Afande Nchimbi na askari wengine waliingia ndani ya nyumba ya Maliki. Walienda chumbani, Nchimbi akainua godoro kuangalia chini ya uvungu wa kitanda alimkuta Maliki kajificha.

"Tulimwamuru atoke, alitii akashuhudia upekuzi ukiendelea. Tulimalizia chumba cha watoto na tulipata nyaraka mbalimbali, hati ya kusafiria ya Maliki na Iddi pamoja na vitambulisho vya benki," alidai shahidi.

Alidai walimchukua Maliki hadi Ofisi ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na wakiwa huko walipata taarifa ya mtuhumiwa mwingine rafiki wa Maliki, anaitwa Iddi kuwa anataka kusafiri kwenda Tanga.

Koplo Gladness alidai kuwa Machi 24, 2022 alfajiri, waliweka kambi Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli Mbezi na walifahamu alikuwa anasafiri na basi la Tashrif.

Anadai kuwa alikuwa anasafiri na basi lenye namba ya usajili T987 DLZ lililokuwa likiendeshwa na Andrew.

Shahidi alidai kuwa alishuhudia Afande Hassan akiwaamuru abiria asishuke mtu, akapanda pamoja na Afande John na Chedi kumtafuta Iddi.

Alidai kuwa walimkuta Iddi amekaa kwenye kiti namba 37 akiwa na kipochi cheusi. Walimshusha ndani ya basi lakini dereva alipoulizwa kuhusu mshtakiwa huyo, alimtaja mshtakiwa mwingine aliyekuwamo ndani ya basi hilo.

Mshtakiwa huyo, Ally Maliki, anadaiwa alipandia Mwembe Yanga Temeke na askari walipanda tena ndani ya basi na kumshusha Ally aliyekuwa amekaa kwenye kiti namba 21.

Shahidi alidai washtakiwa wote walipopekuliwa walikutwa na simu zao pamoja na tiketi za kusafiria na ndani ya kipochi cha Iddi ulikutwa unga uliobainika kuwa dawa za kulevya.

"Machi 25, 2022 nilifunga kielelezo kikishuhudiwa na washtakiwa wote watatu na shahidi huru anaitwa Mashaka, baada ya kufungua Machi 28, mwaka huo, nilipeleka kwa Mkemia Mkuu kwa ajili ya uchunguzi. Sampuli ilipopimwa ilibainika ule unga ni dawa za kulevya kilo 1.02," alidai.

Akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Nehemiah Nkoko, shahidi alikubaliana na Wakili kwamba sheria ya dawa za kulevya inataka basi hilo kukamatwa kisha kupelekwa mahakamani kama kielelezo.

Alidai kuwa wakati washtakiwa wanakamatwa alishuhudia wakishushwa kwenye basi akiwa chini. Pia alidai hakushuulika na suala lolote linalomuhusu mshtakiwa wanne, Mwinyi Mgazija.

Akihojiwa na Jaji Isaya aeleze kwa nini alifunga kielelezo Machi 25 akapeleka Ofisi ya Mkemia Machi 28, Gladness alidai Machi 26 na 27 zilikuwa siku za mapumziko Jumamosi na Jumapili.

Shahidi alimaliza kutoa Ushahidi na shauri liliahirishwa hadi Desemba 4, mwaka huu, kwa ajili ya kuendelea na usikilizaji wa mashahidi wengine.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations @guardian.co.tz*

HABARI KITAIFA

# Hatifungani kukusanya bilioni 150/- za kulipa makandarasi wa barabara

## -Rais Samia aongoza ununuzi, Mpango...

**Na Restuta James**

HATIFUNGANI mpya imezinduliwa nchini. Serikali imesema inakusudia kuitumia kuongeza mtandao wa barabara, ujenzi na ukarabati wa madaraja na makalavati ili kuchochea maendeleo mijini na vijijini.

Hiyo ni hatifungani iliyopewa jina la 'Samia Infrastructure Bond' (Hatifungani ya Samia ya Miundombinu) inayolenga kukusanya Sh. bilioni 150 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara za vijijini na mijini zilizo chini ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA).

Akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, jana wakati wa uzinduzi wa hatifungani hiyo kwenye Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam, alipongeza Benki ya CRDB kwa kuzindua hatifungani hiyo.

Hatifungani hiyo ni mwendelezo wa mauzo ya Mpango wa Muda wa Kati wa Miaka Mitano unaolenga kukusanya Sh. sawa na dola za Marekani milioni 300. Mpango huo wa miaka mitano uliidhinishwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Masoko ya Fedha na Mitaji (CMSA) na katika awamu ya kwanza, Benki ya CRDB iliuza Hatifungani ya Kijani ambayo ilikuwa ya kwanza kwa ukubwa kusini mwa Jangwa la Sahara.

Akizungumza na mamia ya washiriki katika hafla hiyo ikiwamo viongozi wa taasisi za umma na binafsi, wafanyabiashara, wawekezaji na wananchi waliojitokeza kwenye uzinduzi wa Hatifungani ya Samia ya Miundombinu, Dk. Mpango alisema inafurahisha kuona taasisi ya fedha za kizalendo ikiongoza mchakato wa kuwaleta pamoja watanzania na wawekezaji kutoka nje ya nchi kuchangia ujenzi wa miundombinu ya barabara kuchochea maendeleo ya taifa.

"Furaha yangu ya kujumuika katika masuala yanayochochea ustawi wa maendeleo ya taifa letu huwa maradufu ninapoona serikali, taasisi binafsi na wananchi tunaungana kujijenga Tanzania yetu.


"Ninafarijika sana ninapoona taasisi zetu ziko mstari wa mbele kuchochea maendeleo kama ambavyo Benki yetu ya CRDB, kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI na TARURA walivyokuja na hatifungani inayowawezesha Watanzania kuwekeza fedha zao kufanikisha ujenzi wa barabara nchini," alisema Makamu wa Rais.

Kitu kizuri katika hatifungani hiyo, Dk. Mpango alisema ni mkakati wa Benki ya CRDB kuwashirikisha watanzania wote kuendeleza miundombinu ya barabara, hali itakayoipa serikali shinikizo la kuhakikisha inajenga barabara nzuri na imara kadri inavyowezekana.

Makamu wa Rais alisema serikali inafanya kila inaloweza kuhakikisha watanzania wanainuka kiuchumi na kati ya njia za kufanikisha hilo ni kuboresha miundombinu muhimu inayochangia maendeleo ya sekta tofauti.

"Pamoja na juhudi za serikali katika kuboresha miundombinu, tumekuwa na changamoto za malipo kwa wakati. Sasa ninategemea kuona makandarasi wakichangamkia fursa hii kikamilifu.

"Mbali na manufaa kwa nchi na makandarasi, hatifungani hii pia ina faida ya riba ya asilimia 12 kwa wawekezaji kwa kila mwaka kwa miaka mitano ya uhai wake. Riba hii italipwa katika kila robo ya mwaka, hivyo inafanya mwekezaji kuwa na uhakika wa kipato kila baada ya miezi mitatu. Hakika ni uwekezaji mzuri kwa wote wenye nia na uwezo wa kuwekeza," alisema.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akikabidhiwa mfano wa hatifungani baada ya kuwekeza Sh. milioni 100 katika Hatifungani ya Samia ya Miundombinu, baada ya uzinduzi jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela. **PICHA: OMR**

Makamu wa Rais alielekeza TAMISEMI na Benki ya CRDB kuendelea kutoa elimu ya masuala ya fedha na uwekezaji kwa wananchi, ili wanunue hatifungani hiyo na zinginezo zinapotangazwa.

"Utafiti unaonesha zaidi ya asilimia 80 ya watanzania wanaweka akiba kwa ajili ya dharura kama elimu, chakula, matibabu na misiba. TAMISEMI ishirikiane na CRDB kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa hii," aliagiza Dk. Mpango.

Pia alielekeza TARURA kuendelea kubuni mbinu na teknolojia za kisasa katika ujenzi wa barabara kwa kutumia malighafi zinazopatikana nchini.

Vilevile, Makamu wa Rais alielekeza wakala huo kuhakikisha miundombinu inayotekelezwa kwa hatifungani, ikamilishwe kwa wakati na kwa kuzingatia ubora.

Dk. Mpango alisema mtandao wa barabara za lami nchini umeongezeka kutoka Km 13,235.1 mwaka 20 hadi kilometa 15,366.36 mwaka huu.

Alisema bajeti ya TARURA imeongezeka kutoka Sh. bilioni 414.5 mwaka 2019/20 hadi Sh. bilioni 841.2 mwaka 2024/25.

Makamu wa Rais alisema uzinduzi wa hatifungani hiyo ni mwendelezo wa serikali kuimarisha ubia kati ya sekta binafsi na ya umma.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema wanafahamu serikali hutenga mabilioni ya shilingi kwa ajili ya kujenga na kurekebisha barabara zilizoharibika ili kurahisisha ufikishaji huduma kwa wananchi, usafirishaji bidhaa na mazao pamoja na usafiri wa wananchi kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

"Tunajivunia kuja na hatifungani hii maalumu inayolenga kukusanya fedha kwa ajili ya miradi ya miundombinu ya barabara za mjini na vijijini. Kupitia hatifungani hii, tunatarajia kukusanya Sh. bilioni 150 zitakazotumika kuwalipa makandarasi wanaoendelea na watakaokuwa wanajenga barabara," alisema Nsekela.

Kupitia hatifungani hiyo itakayouzwa kwa siku 30 kuanzia jana ilipozinduliwa hadi tarehe 17 Januari 2024, Nsekela alisema Benki ya CRDB inatoa fursa kwa kila mtanzania, zikiwamo taasisi na kampuni kuwekeza kiasi chochote kuanzia Sh. 500,000 huku akitarajia kupokea faida ya asilimia 12 kwa mwaka.

Kwa mtu au taasisi inayotaka kuwekeza, Nsekela alisema anaweza kuipata hatifungani hiyo katika tawi lolote la benki katika zaidi ya matawi 260 yaliyomo nchini au akafanya hivyo katika simu yake ya mkononi kupitia SimBanking ikiwa ni benki ya kwanza barani Afrika kuwezesha wateja na wawekezaji kuwekeza katika hatifungani kidijitali.

"Uwekezaji kwenye hatifungani hii ni salama na wenye faida nzuri. Ukiinunua unakuwa umewekeza kati benki kubwa zaidi nchini yenye uhakika wa kukulipa faida unayoitarajia. Ninamkaribisha kila mtanzania mwenye uwezo kuja kushirikiana nasi kujenga barabara zetu," alisema Nsekela.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Nicodemus Mkama, alisema kuwa kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika awamu ya kwanza, ana imani mauzo ya Hatifungani ya Samia ya Miundombinu nayo yatavuka malengo yaliyokusudiwa.

"Hatifungani ya Kijani ilikusudia kukusanya Sh. bilioni 40 lakini zikapatikana Sh. bilioni 171.82 sawa na asilimia 429.6. Ninaamini rekodi hiyo itafikiwa tena kama si kuvunjwa kwani watanzania wako tayari kujijenga nchi yao. Nitumie fursa hii kuwahamasisha watanzania kuwekeza katika fursa zilizoko katika masoko ya mitaji na dhamana kwani zina uhakika wa kipato," alisema Mkama.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Nchi - TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa mwenye dhamana na TARURA, alisema Benki ya CRDB ndio taasisi pekee iliyoendana na matakwa ya wizara katika mkakati wake wa kutafuta uhakika wa fedha za kufanikisha ujenzi wa barabara nchini.

"Ili kujenga barabara kwa kasi inayotakiwa, fedha nyingi zinahitajika, hivyo wizara iliona ni busara kutafuta vyanzo mbadala vya mapato na hapa nirudie tena kupongeza Benki ya CRDB kwa kuja na ubunifu huu utakaosaidia kwa kiasi kikubwa kupata fedha kwa wakati, hivyo miradi mingi kukamilika kama ilivyopangwa," alisema Waziri Mchengerwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TARURA, Victor Seff, alisema ushirikiano huo ulitolewa na Benki ya CRDB utasaidia kupatikana fedha kwa wakati kuharakisha ukamilishaji miundombinu ya barabara na kutatua changamoto zilizoko katika maeneo tofauti nchini.

"Kazi imebaki kwa makandarasi peke yao kutenda kazi zao kwa viwango vinavyokubalika kujijenga nchi yetu. Hatifungani hii itakusanya fedha za wananchi kwa ajili ya miradi itakayojengwa na wazawa kwa maendeleo ya taifa letu.

"Ni muhimu kwa makandarasi kuonesha weledi katika miradi yote mtakayopewa kuitekeleza. Juhudi hizi za Benki ya CRDB kukusanya fedha kutoka kwa wananchi zinapaswa kuzaa matunda ya barabara imara," alisema Seff.

Katika uzinduzi huo, Makamu wa Rais, alifungua pazia la ununuzi wa hatifungani hiyo kwa kupanda (kununua hatifungani) Sh. milioni 100, huku taasisi za umma, vikundi vya kinamama wajasiriamali na watu binafsi wakijitokeza kuwekeza katika hatifungani hiyo.

Baadaye Dk. Mpango alitangaza kupokea ujumbe kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan, aliyeahidi kuwekeza pia katika hatifungani hiyo kwa kupanda (kununua hatifungani) Sh. milioni 100.

Kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu wa TARURA, Seff, wakala huo unasimamia barabara za wilaya zenye urefu wa kilometa 144,000, madaraja 3,560 na makalavati 80,000.

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bado mapema sana, Yanga isikate tamaa

**WIKI** hii tumeshuhudia michezo mbalimbali ya kimataifa kwa ngazi ya vilabu ambapo hapa nchini timu zetu kubwa za Simba na Yanga nazo zilikuwa uwanjani.

Yanga ilikuwa ya kwanza kucheza Novemba 26 kwenye mchezo wa kwanza hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal ya Sudan.

Watani zao, Simba wenyewe walicheza siku iliyofuata dhidi ya Bravos do Marquiz ya Angola kwenye mchezo wa kwanza pia hatua ya makundi ya kombe la Shirikisho Afrika, michezo yote hiyo ilichezwa kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Ni Yanga ambayo haikupata matokeo mazuri kwenye uwanja wake wa nyumbani baada ya kukubali kipigo cha mabao 2-0 huku watani zao Simba wakiibuka na ushindi wa bao 1-0.

Matokeo hayo yameibua hisia tofauti miongoni mwa mashabiki wa Yanga ambao wanaona timu yao haifanyi vizuri na imeanza vibaya kwenye michuano hiyo ambayo msimu uliopita ilifika mpaka hatua ya robo fainali.

Wengi wao wanaona timu haijacheza vizuri na wapo wanaoona kuondoka kwa aliyekuwa kocha wao, Miguel Gamondi ni sababu iliyochangia timu hiyo kufungwa na Al Hilal.

Maumivu hayo yamekuja pia baada ya Yanga kupoteza michezo miwili mfululizo ya Ligi Kuu Tanzania Bara na sasa mashabiki wameanza kuikatia tamaa timu yao.

Lakini kiuhalisia na kwa maana halisi ya mpira wa miguu, ni mapema sana kwa mashabiki na wapenzi wa Yanga kuanza kuikatia tamaa timu hiyo ambayo ndio kwanza wamecheza mchezo wao wa kwanza wa hatua hiyo ya makundi.

Kupoteza alama tatu kwenye mchezo wa kwanza bado sio kigezo cha timu hiyo kufanya vibaya kwenye hatua hiyo kwa sababu bado wana michezo mingi mbele yao.

Kikubwa kwa sasa Yanga wanapaswa kutuliza akili na kujipanga upya kuelekea kwenye mchezo wao wa pili ambao watacheza ugenini dhidi ya MC Alger ya Algeria.

Wachezaji na benchi la ufundi wanapaswa kufahamu michezo inayofuata ndio muhimu zaidi kwao katika kufikia malengo yao ya kufuzu hatua ya robo fainali.

Matokeo ya mchezo uliopita yaishie uwanja wa Benjamin Mkapa na sasa ni kipindi cha kufanya maandalizi na kujipanga vizuri kabla ya mchezo unaofuata ambao utachezwa Desemba 7 nchini Algeria.

Matokeo mazuri watakayoyapata kwenye mchezo huo yatainua molari kwa wachezaji na kuanza kurudisha imani ya mashabiki wao katika kuikimbilia hatua ya robo fainali.

Mashabiki hawapaswi kukata tamaa na kuingiwa unyonge baada ya mchezo huo mmoja, bado kuna michezo mingine mbele ambayo kama Yanga watachanga karata zao vizuri wananafasi ya kutinga robo fainali.

Nipashe tunaamini Yanga bado ipo kwenye nafasi ya kufanya vizuri kwenye kundi lake ambalo mbali Al Hilal pia kuna timu za MC Alger na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Kikubwa ni kujipanga na kujiandaa kikamirifu kuelekea kwenye mchezo wao wa Desemba 7 dhidi ya MC Alger, hakuna kisichowezekana kwenye mpira, Yanga inaweza kupata ushindi ugenini na kushangaza wengi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Adam Fungamwango

# Wanachama, mashabiki Yanga wawe na subira

**WANACHAMA** na mashabiki wa Yanga kwa sasa hawaelewi wamlaumu nani. Wengine wanawalaumu wachezaji. Wapo wanaowalaumu viongozi. Hii yote ni kwa sababu ya kufanya vibaya kwenye michezo mitatu mfululizo iliyopita.

Ilianza kwa kufungwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, mechi iliyochezwa, Novemba 2 mwaka huu. Mashabiki wakaona kama ni bahati mbaya tu.

Novemba 7, mwaka huu hali ilikuwa mbaya zaidi pale ilipopokea kipigo cha mabao 3-1 dhidi ya Tabora United.

Hapo ndipo baadhi ya mashabiki walianza kushtuka na kuona kabisa kuna kitu kisicho cha kawaida ndani ya timu au klabu.

Ni kwa sababu si kitu cha kawaida kwa timu kubwa kama za Simba na Yanga kupoteza michezo miwili mfululizo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Si kwa misimu ya hivi karibuni hata miaka iliyopita, timu hizo hazikuwa na kawaida ya kupoteza michezo miwili mfululizo. Labda inaweza kufungwa na mechi inayofuata kutoa sare. Au kutoa sare mechi inayofuata kufungwa.

Ndiyo maana mashabiki wa Yanga wakawa wakali mno, kwa sababu hawajawahi kukutana na hali kama hii.

Kingine ni kufungwa idadi kubwa ya mabao ya timu ya daraja la kati kama Tabora United. Yanga kufungwa mabao matatu na Simba si kitu kigeni sana, lakini si timu nyingine kwenye Ligi Kuu.

Mara nyingi timu za madaraja ya kati au ya chini wakishatangulia kwa bao 1-0 dhidi ya timu kubwa, watahakikisha hawapandi tena mbele kushambulia, badala yake kuzuia na kupoteza muda hadi mechi imalizike.

Ndiyo maana si mara nyingi kukuta Simba au Yanga zinafungwa idadi kubwa ya mabao na timu hizo, badala yake hupoteza kwa bao 1-0. Hii ya Tabora United pia ilikuwa kama 'sapraizi.'

Baadhi ya mashabiki wa Yanga wanawatuhumu wachezaji wao kuwa wamebweteka kwa kupata majina makubwa, wameshakuwa mastaa, sasa wamevimba vichwa na hawajitumi tena, huku wakiwa wazee wa starehe, na hii inasababisha viwango vyao kupungua.

Wapo wanaowalaumu viongozi kwa kuwadekeza baadhi ya wachezaji wanaojiona mastaa, wakiwaachia wazurule, wasikae kambini, hivyo kupoteza ubora wao. Kuna wanaowalaumu viongozi kwa kumtimua kocha Miguel Gamondi akisema haikuwa na ulazima wowote, wao wakiona kama hana kosa lolote, kilichotokea ni mambo ya mpira tu.

Wao wanaamini kuwa viongozi wamefanya hivyo ili tu kuficha madhaifu yao ili wanachama na mashabiki waamini kuwa tatizo ni kocha.

Binafsi sipingani na makundi yote hayo. Inawezekana kila kundi lipo sahihi, au moja kati ya hilo. Au yote yasiwe sahihi, ila ushauri wangu ni kwamba wanachama na mashabiki watulie ili kuwafanya viongozi nao watulie na kusaka kile kinachoitafuna timu kwa sasa. Wanachama na mashabiki walianza kuwa wakali na kuwaanyooshea vidole, kitakachotokea ni kuwa hawatokuwa watulivu na hata maamuzi yao wanaweza kuyafanya kwa woga, mihemko ili kuwaridhisha wao, lakini kumbe ndiyo wanaharibu zaidi.

Najua kuwa kufugwa kunauma, hasa kwa timu kubwa kama hii, lakini sidhani kama viongozi wao wamelala.

Ni lazima watakuwa wanatafuta nini kinawatafuna. Kama ni wachezaji wameshuka kiwango, au wanakesha kwenye starehe, umri umekwenda, basi wao ndiyo wataamua nini wafanye na watafanya kwa manufaa ya klabu, wanachama na mashabiki kwa sababu wao ndiyo waliopewa mamlaka.

Kwa maana hiyo wanachama na mashabiki wa Yanga watulie, wasiwachanganye viongozi wao ili nao watulie wafanye maamuzi kwa manufaa ya klabu.

HABARI KITAIFA

# INEC yaonya kujiandikisha mara mbili

**Na Mary Mosha,** MOSHI

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) imetoa onyo kwa wananchi kujiandikisha kupiga kura mara mbili katika daftari la Kudumu la Wapigakura.

Imesisitiza kuwa kitendo hicho kinaweza kusababisha mhusika kufungwa jela miezi isiyopungua sita au kulipa faini ya Sh. 500,000 au vyote kwa pamoja.

Makamu Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji (mstaafu) Mbarouk Salimu Mbarouk, aliyasema hayo jana mjini hapa wakati akifungua mkutano wa tume na wadau wa uchaguzi kuhusu uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura.

Jaji Mbarouk alisema kujiandikisha kupiga kura zaidi ya mara moja ni kosa kisheria na kuwataka wadau wa uchaguzi kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kujiandikisha.

"Mfumo tuliokuja nao kwa sasa ni rafiki wa ufuatiliaji watakaopiga kura mara mbili, hivyo ni marufuku kwa mwananchi kujiandikisha na kupiga kura mara mbili.

Wadau mbalimbali, wakiwamo wanasiasa wa vyama vyote, hakikisheni mnatoa elimu kwa wananchi juu ya kosa hili kwani wakifanya hivyo, wanavunja Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Kifungu cha 114 na tume haitamvumilia mtu yeyote atakayefanya hivyo," alisema.

Akiwasilisha mada kwa niaba ya Mkurugenzi wa Uchaguzi, Mkurugenzi wa Huduma za Kisheria wa INEC, Selemani Mtibora, alisema mpigakura ambaye ana kadi zilizotolewa zamani na ambazo ni za karatasi, atalazimika kujiandikisha upya katika daftari.

Mtibora alisisitiza kuwa mpigakura ambaye ana kadi ambazo zimeandikishwa mwaka 2015 na 2020, hatahusika na uboreshaji huo wa daftari isipokuwa wale wenye matatizo mbalimbali yakiwemo ya kupoteza kadi, kuhamisha taarifa na kuwaondoa watu waliokosa sifa za upigaji kura.

Akichangia mada hiyo, Mkuu wa Magereza Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishina Msaidizi Mwandamizi (SACP) Leonard Melkior, aliiomba tume hiyo kuweka utaratibu maalumu kwa wafungwa na mahabusu ili kushiriki katika uandikishwaji huo.

Mmoja wa wawakilishi wa vyama vya siasa mkoani, Katibu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Basil Lema, aliomba tume kuruhusu mawakala zaidi na wa akiba ili kuondoa chuki na mikanganyiko isiyo ya lazima kwa wananchi.

Mkoa wa Kilimanjaro unatarajiwa kuandikisha wapigakura wapya 180,540 ikiwa ni ongezeko asilimia 18 ya wapigakura 1,009,729 waliomo kwenye daftari, hivyo kuwa na jumla ya wapigakura 1, 190,266.




Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Jaji (Rufaa) Jacobs Mwambegele, akizungumza wakati akifungua mkutano wa siku moja wa Tume na Wadau wa Uchaguzi, mkoani Arusha jana, ikiwa ni maandalizi ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura unaotarajia kuanza Desemba 11 hadi 17, 2024. Wadau hao ni pamoja na viongozi wa vyama vya siasa, dini, wawakilishi wa asasi za kiraia, wahariri wa vyombo vya habari, waandishi wa habari, maofisa habari wa mikoa na halmashauri, wawakilishi wa makundi mbalimbali ya vijana, watu wenye ulemavu, wanawake na wazee wa kimila. Kulia ni Mkurugenzi wa Uchaguzi wa INEC, Kailima Ramadhani. **PICHA: INEC**

# Waziri akemea rushwa, udokozi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana, amezindua rasmi Bodi ya Magavana ya Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori MWEKA na kusisitiza chuo hicho kuendelea kutoa mafunzo bora yanayokidhi mahitaji kulingana na vipaumbele vya taifa.

Pia amekitaka chuo kupiga vita vitendo vya rushwa, ubadhirifu, wizi na unyanyasaji wa kijinsia.

Chana alisema hayo jana wakati wa akizindua bodi hiyo mkoani na kuielekeza kuweka mikakati ya kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka ndani na nje ya nchi.

"Mimi pamoja na uongozi mzima wa wizara tuna imani kubwa nanyi kuwa kwa kutumia weledi, ujuzi na uzoefu wenu mtakisaidia chuo hiki ambacho kwa miaka mingi kimekuwa kiwanda kikubwa na muhimu cha kuzalisha wataalamu wa wanyamapori na utalii si ndani ya Tanzania tu, bali duniani kote," alisema.

Waziri aliitaka pia bodi hiyo kuandaa kozi mahsusi zitakazozingatia matumizi ya teknolojia kwenye usimamizi wa wanyamapori na utalii kwa lengo la kulinda na kuendeleza maeneo ya hifadhi kwa mifumo wa kidijitali hasa katika malipo ya kifuta jasho, udhibiti wa moto na ulinzi wa misitu.

Pia aliielekeza bodi hiyo kuimarisha miundombinu ya chuo na vitendea kazi ili viendane na mahitaji ya elimu inayotolewa na kuimarisha utafiti na ushauri wa kitaalamu kwa lengo la kujibu changamoto zinazokabili sekta za uhifadhi na utalii nchini na katika nchi za kikanda.

Mwenyekiti wa Bodi ya Magavana ya Mweka, Prof. Yunus Mgaya, aliahidi kuwa yeye na timu yake watatekeleza majukumu kwa weledi, ufanisi na tija ili kufikia kwa matarajio na malengo ya serikali.

"Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wangu tutahakikisha tunarejea kuandaa mitaala na kuongeza program za masomo zinazojibu changamoto mbalimbali katika sekta ya mazingira, maliasili na utalii.

"Pia tutakifanya chuo kukubalika na kuwa chuo mahiri cha kutoa mafunzo katika taaluma mbalimbali za uhifadhi, maliasili na utalii. Hili tunalenga hasa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na nchi wanachana wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika( SADC)," alisema.

Uzinduzi huo ulihudhuriwa na Mkuu wa Chuo hicho ambaye pia ni Katibu wa Bodi, Prof. Jafari Kideghesho, wajumbe wa bodi, uongozi wa chuo na viongozi wa serikali ya wanafunzi.

# Waziri atema cheche bodi mpya Taasisi ya Uongozi

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, ameitaka bodi mpya ya Taasisi ya Uongozi kutimiza dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kupata sura ya bara la Afrika katika kujenga uwezo wa viongozi wake.

Simbachawene aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa bodi mpya ya taasisi hiyo.. Alisema alisema moja ya sababu za kuanzishwa kwa taasisi hiyo ni kujenga uwezo wa viongozi wa bara la Afrika kuwa na mipango na mawazo endelevu ya maendeleo katika kutunza rasilimali na kukuza uongozi.

Alisema Rais Samia amechagua bodi nzuri ambayo ina mchanganyiko wa watu wa nchi mbalimbali ambao watakuja na kitu kipya ili kutekeleza malengo yaliyojiwekea katika kujenga uwezo wa viongozi Afrika waliopo, wajao na watu mbalimbali ikiwamo viongozi waliopo madarakani na wale waliopo katika maeneo mengine.

"Nimezindua bodi mpya ya Taasisi ya Uongozi ambayo ni taasisi ya kikanda na taasisi ya Afrika ambayo bodi yenyewe imeteuliwa na Rais kwa mujibu wa sheria ya taasisi yenyewe.

"Rais amewateua na amewapongeza kwa kupata nafasi hii kwani Taasisi ya Uongozi ni taasisi ya Afrika na ina bahati Tanzania na Finland zinachangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya taasisi hii ambayo wengine wanaingia kulingana na programu zinazotolewa na taasisi ambazo ni nyingi,"alisema.

Simbachawene alisema shughuli zinazofanywa na taasisi ni pamoja na uandaaji wa midahalo mikubwa inayofanyika hata na viongozi wakubwa wa nchi ambao ni marais kushiriki katika midahalo hiyo na pia kutoa mafunzo kwa viongozi vijana na viongozi waliopo katika maofisi katika taasisi mbalimbali ili kutoa huduma zinazokwenda na wakati.

Mwenyekiti mpya wa bodi hiyo ambaye ameingia kipindi cha pili, Balozi Ombeni Sefue, alisema kuzinduliwa kwa bodi hiyo ambayo kwa sasa ni ya tano ni uendelezaji wa kazi nzuri zilizofanywa na bodi iliyopita iliyokuwa na mikakati mbalimbali inayoongoza kazi za taasisi.

Alisema bodi hiyo mpya inachukua malengo ya serikali yaliyoachwa na bodi ya zamani kwa kuhakikisha wanayatekeleza kwa mikakati iliyopo.

"Mpango mkakati wetu uliopo sasa ni ule wa bodi iliyopita ambao kwa sasa una mwaka kumalizika, hivyo kazi mojawapo ya bodi hii ni kuandaa mkakati utakaofuata baada ya mafanikio yaliyotajwa hapa pamoja na utekelezaji wa mkakati ambayo ipo ikiwamo kuongeza programu mpya, kuandaa wanawake katika uongozi, programu ya kuboresha utendaji wa mashirika ya umma na programu maalum ya usimamizi wa mashirika ya umma ambayo ni programu mpya kwa kushirikiana na ofisi ya Hazina," alisema.

# FCC kutoa elimu Siku Ushindani Duniani

**Na Faustine Feliciane**

TUME ya Ushindani wa Biashara (FCC) imesema itaendelea kutoa elimu kwa wadau mbalimbali kuhusu njia nzuri ya ushindani katika biashara.

Mkurugenzi Mkuu wa FCC, Dk. William Erio, alisema juzi Dar es Salaam kuwa tume imeandaa semina kwa kada mbalimbali katika kuadhimisha Siku ya Ushindani Duniani ambayo hufanyika kila ifikapo Desemba 5 ya kila mwaka.

"Kwa mwaka huu maadhimisho haya yatafanyika Dar es Salaam na tunategemea Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Suleiman Jafo, atakuwa mgeni rasmi.

Mambo mengi tumeandaa ikiwa ni pamoja na semina kwa wanafunzi wa vyuo, wadau wa sheria na wafanyabiashara ambayo tutaitoa Desemba 2 na 3," alisema.

Dk. Erio alisema siku moja kabla ya maadhimisho, wanatarajia kutoa elimu kwa umma kupitia vipindi vya redio katika vituo mbalimbali.

Pia alisema siku ya maadhimisho, wanatarajia kufanya kongamano la wafanyabiashara na wadau wengine na mada mbalimbali zitatolewa.

"Lengo la kufanya haya yote ni kuonyesha Watanzania na wadau wengine kazi zinazofanywa ma FCC na kile ambacho serikali inakifanya katika kuweka mazingira mazuri ya biashara," alisema.

Dk. Erio alisema kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu kuwa ni 'Sera ya Ushindani Zinaweza Kupunguza Utofauti wa Ushindani wa Kibiashara'.



Meneja Wakala wa Vipimo (WMA), Henry Msambila (kulia), akitoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya vipimo katika ufungashaji wa vinywaji vinavyozalishwa kwa kutumia zao la zabibu katika Maonesho ya Kimataifa ya Utalii Zabibu, katika viwanja vya Reli, jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# WMA yasisitiza vipimo sahihi kwa wauza mvinyo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Dodoma, imewahimiza wajasiriamali na wafanyabiashara wanaojihusisha na uuzaji wa mvinyo na usindikaji wa bidhaa zinazotokana na zao la zabibu kuzingatia matumizi sahihi ya vipimo katika biashara zao.

Wito huo ulitolewa jana na Meneja wa WMA Mkoa wa Dodoma, Karim Zuberi, alipowatembelea wauzaji wa mvinyo wanaoshiriki katika Tamasha la Dodoma Zabibu Tourism International Fair kwenye Viwanja vya Reli Dodoma Mjini. WMA ni moja ya taasisi zinazoshiriki katika tamasha hilo.

Zuberi alisema Mkoa wa Dodoma unaongoza kwa kilimo cha zabibu nchini na zao hilo ni moja ya mazao ya kimkakati.

Aliwataka wakulima na wafanyabiashara kujikita katika uzalishaji wenye tija kwa kuhakikisha zabibu zinazofungashwa na kuuzwa kwenye maduka mbalimbali na zile zinazo safirishwa kwenda nchi jirani zinapimwa na kufungashwa kwa kuzingatia vipimo sahihi.

Alisema wale wanaoongeza thamani kwa kutengeneza mvinyo kadharika wafungashe kwa kutumia vipimo sahihi ili kuwalinda walaji.

"Katika Jiji letu la Dodoma wafanyabiashara wengi hulionGezea thamani zao la zabibu kwa kutengeneza mvinyo (wine) na hufungashwa kwenye madumu na chupa zenye ujazo tofauti hivyo nawaasa wafanyabiashara kutumia vipimo sahihi katika uzalishaji wao kama ambavyo Sheria ya Vipimo Sura Na.340 inavyoelekeza.

"Mkishatumia vipimo sahihi katika kufungasha bidhaa hii ya mvinyo, hakikisheni mmeweka alama ya maandishi au kibandiko chenye kuonesha ujazo wa mvinyo katika kifungashio husika. Hii itachagiza kuleta haki baina ya muuzaji na mnunuzi kwa kujua kiasi sahihi cha bidhaa anayonunua," aliongeza Zuberi.

Alisema WMA imeendelea na uboreshaji wa huduma zake kwa kutimiza majukumu yake kwa ufanisi na kushirikiana na wadau wa vipimo pamoja na wananchi kwa ujumla kama kushiriki katika maonesho, hafla na mikutano mbalimbali yenye tija katika kuinua sekta ya vipimo nchini.

Zuberi aliwakaribisha wananchi wa Mkoa wa Dodoma kutembelea banda la WMA katika maonesho hayo ili kuendelea kujifunza kuhusu huduma zinazotolewa na wakala ikiwa ni pamoja na eneo la uhakiki wa dira za maji mpya pamoja na zile ambazo zipo kwenye matumizi, mita za umeme na vipimo vingine.

Mjasiriamali wa bidhaa ya mvinyo, Zaituni Ramadhani, aliishukuru WMA kwa kutembelea bidhaa zake na kumpa ushauri wa kitaalamu wa namna ya kuboresha ufungashaji wa bidhaa zake ikiwa ni pamoja na kuweka taarifa za kiujumla kuhusu ufungashaji wa bidhaa yake.

# Tisa waliosombwa na maji wazikwa Tarime

**Na Timothy Itembe,** TARIME

MKUU wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi, ameongoza mamia ya wakazi wa Tarime mkoani Mara kuaga na kupumzisha miili ya watu tisa waliofariki dunia kwa kusombwa na mafuriko ya maji katika Mto Mori.

Tukio hilo lilitokea Novemba 24, mwaka huu, kutokana na mvua iliyonyesha majira ya saa 4:00 usiku na kusomba nyumba mbili zilizokuwa zimejengwa kando ya Mto Mori na kusababisha vifo hivyo vya watu kutoka familia mbili.

Akizungumza wakati wa kuaga miili hiyo, Kanali Mtambi aliwataka viongozi mbalimbali wakiwamo viongozi wa serikali, viongozi wa kimila kutoa elimu kwa watu wanaoishi mabondeni kuhama mara moja kabla ya kufikiwa na madhira ya namna hiyo.

Mtambi alisema uhamishaji wote ambao wanaishi mabondeni unatakiwa kutumia nguvu kama wameshindwa kuhama kwa hiari.

Alisema kuwa maji hayasahau mkondo wa kupita na kuwa maji hayo hata yakae muda mrefu mvua itakaponyesha, yatapita kulekule yalikozoea.

Waliofariki dunia katika mafuriko hayo ni Rebeka Omolo (29), Benesoni Omolo (12), Fransinsca Awuor (4), Stell Anyango (30), Salome Omondi (15), Thobias Ochola (1), Frorence Akorhi (55) na Winfrida Atieno (18).

Mkuu wa Wilaya Tarime, Meja Edward Ngowele, alisema wilaya iko salama na wananchi wametoa ushirikiano mkubwa katika tukio ambalo liliwapata wananchi wa Mtaa wa Bugosi, Kata ya Nyamisangura.

Mbunge wa Tarime Mjini, Michael Kembaki, alipongeza ushirikiano wa watu wa Bugosi waliouonesha baada ya wenzao kukumbwa na mkasa huo na kuwataka waombolezaji kuendelea kuwa na moyo huo huo wa ushirikiano.





# TGNP yawezesha mafunzo ya jinsia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP) umeiwezesha mafunzo Menejimenti ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (NAOT) kuzingatia masuala ya kijinsia wakati wa kufanya ukaguzi ili kuimarisha uelewa wa masuala ya jinsia.

Mwezeshaji wa Mafunzo hayo kutoka TGNP, Mary Nsemwa, alisema mbali na kuimarisha uelewa wa usawa wa kijinsia mafunzo hayo pia yataimarisha namna ya kuweka vipaumbele vya kijinsia katika mipango na bajeti kwa kuzingatia malengo, sera, miongozo na kuweka nyenzo za ukaguzi wa miradi ya maendeleo.

Alisema malengo mengine ni kujadili umuhimu wa kuzingatia usawa na kuwa na mtazamo wa kijinsia katika uandaaji wa mipango, miongozo na shughuli za NAOT kama inavyoelekezwa kwenye mwongozo wa bajeti ya mwaka 2024/25.

"Mafunzo haya ni muhimu kwa kuwa yatashirikisha uzoefu wa kitaasisi kuhusu masuala ya kijinsia yatakavyoelekezwa kupitia miongozo ya NAOT na changamoto zake ikiwa ni pamoja na kuweka mikakati ya utekelezwaji na kuboresha maeneo muhimu ya kijinsia katika mipango, bajeti na uandaaji wa sera," alisema.

Alisema ikiwa ofisi hiyo itafanya ukaguzi unaozingatia jicho la jinsia itasaidia fedha na rasilimali za umma kutumiwa kwa usawa na haki kwa makundi yote, ikiwa ni pamoja na wanawake, wanaume na makundi mengine yenye mahitaji maalum.

"Ukaguzi wa aina hii unahakikisha kwamba sera, miradi na huduma za serikali zinachangia kupunguza au kuondoa tofauti za kijinsia na kuwa na athari chanya kwa wanawake na wanaume kwa njia sawa," alisema.

Pia alitaja maeneo ambayo yanapaswa kutazamwa wakati wa kuchunguza kuwa ni pamoja na ulinganifu wa bajeti kwa kuchunguza kama bajeti za serikali zinatengwa kwa usawa kwa miradi inayolenga kufadhili masuala ya jinsia, kama vile elimu kwa wasichana, huduma za afya za uzazi, na miradi ya kiuchumi kwa wanawake.

Alisema eneo lingine ni usawa katika ajira na utumishi wa umma ambapo NAOT inapaswa kuchunguza kama kuna usawa katika ajira na ikiwa wanawake na wanaume wanapata fursa sawa katika serikali na sekta za umma. "Ikiwa ni pamoja na kuangalia kama miradi na programu za serikali zinachukua hatua madhubuti za kuondoa ukosefu wa usawa wa kijinsia na kuzingatia mahitaji ya kila jinsia," alisema.

Awali, akizungumza kwenye ufunguzi wa mafunzo hayo Kaimu Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Benja Majura, alipongeza namna ambavyo TGNP, inavyofanya kazi hasa katika masuala ya kijinsia.

Hata hivyo, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwani yatakuwa chachu kwenye kuongeza uelewa wa namna ya kuweka bajeti ya mlengo wa kijinsia.

# Wapewa mbinu kuepuka tatizo afya ya akili

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WATUMISHI wa umma wametakiwa kutumia muda wao mwingi katika shughuli za kujiingizia kipato baada ya kazi za ofisini ili kupunguza tatizo la afya ya akili baada ya kustaafu.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, aliwasihi watumishi hao alipozungumza nao jana katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida. Watumishi hao walikuwa wakipatiwa mafunzo maalum kuhusu udhibiti wa virusi vya Ukimwi (VVU) na UKIMWI na ugonjwa wa afya ya akili kwa watumishi wa umma mahali pa kazi.

"Tukapime afya zetu kwa kupima magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza. Pia ni vyema kufanya mazoezi ya viungo mara kwa mara ili kuuweka mwili mbali na magonjwa," alisema.

Aliwasisitiza watumishi kuepuka mazingira yote yanayoweza kusababisha wapate maambukizi ya VVU huku akitaka kuwa na uthubutu wa kupima afya zao katika magonjwa ya kuambukiza na yale yasiyoambukiza ili kufahamu hali zao vyema.

Naye Mratibu wa Ukimwi Mkoa wa Singida, Dk. Lewis Rwegayula, aliwataka watumishi kumaliza majukumu yao kwa wakati husika ili kuyamudu vyema mazingira ya kazini na baada ya kazi.

Alisema watumishi wayatambue mahitaji ya mabosi wao na kuyatekeleza vema ili kuepusha migogoro kazini itakayoweza kuwasababishia tatizo la afya ya akili.

"Ni vyema pia kwa viongozi kuzitambua tabia za wasaidizi wao ili kufahamu vyema namna gani watawaongoza na kuwasimamia katika utendaji wao wa kazi. Kila mmoja atambue upungufu wake na kuufanyia kazi ili kutokuwa sababu kwa wengine kupata tatizo la afya ya akili," alisema.

Dk. Rwegayula aliwasihi watumishi kuepuka kutumia dawa ambazo hawajaelekezwa na daktari kwani nazo huchangia tatizo la afya ya akili.

Kaimu Katibu Tawala Msaidizi, Sehemu ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe, Dk. Shilla Mwashiuya, aliwataka watumishi kuwashauri wenzao wenye tatizo au dalili za afya ya akili ndani na nje ya ofisi kwa kuwatia moyo wahusika na kuwasaidia pale inapowezekana na sio kuwavunja moyo.

Awali Meneja wa Mradi kutoka USAID AFYA YANGU, Dk. Said Mgeleka, alisema takwimu zinaonyesha kuwa jinsia ya kiume imekuwa nyuma katika kupima VVU na Ukimwi kwa kuwa kati ya wateja 27,678 walioko kwenye huduma za matibabu; wanaume ni 8,581 sawa na asilimia 31 pekee huku wanawake wakiwa 19,097.

"Kundi linaloongoza kwa maambukizi ya VVU na UKIMWI ni watu walioko katika ndoa. Sababu kuu ikiwa ni kuwa na mpenzi zaidi ya mmoja huku kata za Mandewa na Misuna zikitajwa kuongoza kwa idadi ya maambukizi," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule (wa tatu kushoto), akikabidhi kadi ya Afya ya ICHF kwa Nasri Azizi aliyejiweka wazi kuwa ni mwathirika wa virusi vya Ukimwi, ambayo ni maalumu kwa waathirika, ili waweze kukidhi huduma za afya, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani kiwilaya katika viwanja vya Tanganyika Packers, Dar es Salaam jana. Wengine ni Naibu Meya Manispaa Kinondoni, Michael Urio (kushoto) na (wa pili kushoto) ni Katibu Tawala Wilaya hiyo, Warda Obathany. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mimba za utotoni zapungua, matumaini mapya

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MIMBA za ututoni kwa wasichana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 19 mkoani Dodoma, zimepungua kutoka asilimia 39 mwaka 2015/16 hadi asilimia 22.7 kwa mwaka 2022.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alibainisha hayo juzi wakati wa hafla ya kufunga mradi wa Connect uliotekelezwa ndani ya miaka mitano na Shirika lisilo la kiserikali la Save the Children katika wilaya za Bahi na Kongwa.

Senyamule alisema kwenye utafiti wa kitaifa uliofanywa mwaka 2015/16 kuangalia mimba za utotoni, mkoa wa Dodoma ulikuwa na asilimia 39 kiwango ambacho ni kikubwa kulinganisha na kile cha kitaifa ambacho kilikuwa asilimia 27. "Takwimu za kitaifa zinaonyesha kuwa asilimia 27 ya wasichana wa umri kati ya miaka 15 hadi 19 tayari wamepata ujauzito na kwa mkoa wa Dodoma ilikuwa asilimia 39 kwenye utafiti wa kitaifa wa mwaka 2015/16 kiwango ambacho ni kikubwa zaidi ya kiwango cha kitaifa ndiyo maana mkoa tuliamua kutekeleza mikakati ya kupunguza changamoto hii," alisema Senyamule.

Alisema jitihada hizo zimeleta tija na kusababisha kufikia asilimia hiyo ambayo itaendelea kupungua kutokana na serikali ya mkoa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuendelea kupiga vita mimba za ututoni katika maeneo mbalimbali nchini. Naye Kaimu Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Save the Children, Anatoli Rugaimukamu, alisema mafanikio yaliyopatikana kwenye mradi wa Connect ni pamoja na kuwajengea uwezo wahudumu wa afya ngazi ya jamii wapatao 100 ambao wamefanikiwa kuwafikia zaidi ya kinamama vijana 5,776.

Mbali na hilo pia wametoa mafunzo kazini kwa wahudumu 253 kwenye vituo vya afya 31 katika wilaya za Bahi na Kongwa mkoani hapa, lengo ikiwa ni kuhakikisha wakinamama wanapata elimu juu ya njia za kisasa za uzazi wa mpango baada ya kujifungua. Alisema wahudumu hao wa ngazi ya jamii wataendelea kutoa elimu kwa kinamama kuhusu umuhimu wa kutumia njia za kisasa za uzazi wa mpango, ambazo zitawasaidia kuendelea na shughuli mbalimbali, ikiwamo ujasiriamali wanaofanya ili kujiinua kiuchumi. "Mradi huu umeleta matokeo chanya kwa jamii katika wilaya ambazo umetekelezwa mkoani hapa na hii imepelekea kinamama wengi vijana wanaotumia njia za kisasa za uzazi wa mpango baada ya kujifungua," alisema Rugaimukamu.

Devotha Charles, mkazi wa wilaya ya Kongwa alisema mradi huo umesaidia kinamama wengi vijana kutambua umuhimu wa kutumia njia za uzazi wa mpango ambazo zinawasaidia jamii kulea watoto vizuri kwa kufuata maelekezo wanayopewa na wataalamu wa afya.

Alisema ndani ya miaka mitano ya utekelezaji wa mradi huo kumechangia kinamama wengi kuhudhuria kliniki kupata elimu ya uzazi wa mpango ambayo husaidia wanawake kuendelea na shughuli zao za kila ili kujiinua kiuchumi wao na familia zao. Hata hivyo, ameomba elimu ya njia za kisasa za uzazi wa mpango iendelee kutolewa kwa wanawake ili kuisaidia jamii kujua umuhimu wa kutumia njia hiyo baada ya kujifungua.



## Kasi ukataji miti yaongezeka Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, amesema kasi ya ukataji miti kutokana na shughuli za kijamii na ongezeko la idadi ya watu linalosababisha na shughuli za ujenzi wa nyumba za makazi imeongezeka.

Shamata aliyasema hayo katika Baraza la Wawakilishi Chukwani, alipokuwa akijibu suala la Mwakilishi wa Mwanakwerekwa, Ameir Abdallah Ameir, aliyetaka kujua tathmini juu ya ukataji wa miti kwa ajili kutengeneza samani.

Alisema tathmini zinaonesha kuwa kwa kipindi kilichoanzia Julai 2018 hadi Agosti, mwaka huu, miti 6,994 imeruhusiwa kukatwa na kati ya hiyo 5,945 ni miti ya matunda.

Pia alisema takwimu zinaonesha kuwa asilimia 85 ya miti iliyoombewa na kuruhusiwa kukatwa ni miti ya matunda.

"Ikumbukwe kuwa Wizara ya Kilimo hutoa ruhusa ya kukata miti katika maeneo ambayo Mamlaka zinazohusika na mipango miji zimetoa viwanja kwa ajili ya nyumba za kuishi na miradi ya maendeleo," alisema.

Hata hivyo, alisema ujenzi holela usiofuata taratibu pia umechangia kasi ya ukataji wa miti hiyo ya matunda.

Kutokana na hali hiyo, Wizara ya Kilimo ina jukumu la kuhifadhi na kusimamia rasilimali za misitu na inaendelea kufanya tathmini kwa lengo la kudhibiti kasi ya ukataji wa miti iliyopo.

Pia alisema kwa mujibu wa tathmini hali hii isipodhibitiwa itasababisha kuongezeka kwa athari za kimazingira zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi ikiwamo kutoweka kwa baioanuai, kuongezeka kwa hali ya joto, uvamizi wa maji ya bahari katika maeneo ya kilimo na makazi, ukame, kunyesha mvua isiyotabirika inayoweza kusababisha mafuriko, maradhi ya mlipuko na maafa.

# SMZ kusimamia upatikanaji sera ya habari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar imesema itaendelea kusimamia vyema upatikanaji wa sera mpya ya habari na maofisa habari ili kulinda haki na masalahi ya wanahabari.

Waziri wa Wizara hiyo, Tabia Maulidi Mwita, alisema hayo jana katika ukumbi wa Shekhe Idriss Abdul Wakil, Kikwajuni, alipokuwa akizindua Jumuiya ya Maofisa Habari na Mawasiliano Zanzibar (ZICCO).

Alisema wanahabari ni wanatasnia muhimu katika taifa katika kutangaza mafanikio ya serikali kwa jamii hali inayosababisha wananchi kujenga imani na serikali yao.

Waziri Tabia alisema atahakikisha anasimamia maslahi ya wanahabari na maofisa habari katika taasisi binafsi hatua ambayo itaisaidia taifa kukuza tasnia hiyo.

Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Charles Hillary, aliwataka maofisa habari kutimiza majukumu yao kwa usahihi kwa kutangaza maendeleo na kazi za taasisi zao.

Pia aliwataka kutokutoa visingizio vya ukosefu wa vifaa vya kufanyia kazi bali wanapaswa kufika kwa wakuu wa taasisi zao kupatiwa vifaa.

Mwenyekiti wa ZICCO, Raya Hamad Suleiman, alitaka serikali kuwapatia nafasi za mafunzo maofisa habari ili kuendana sambamba na mabadiliko ya kasi ya maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Uzinduzi wa ZICCO uliambatana na mafunzo kwa maofisa habari na mawasiliano, wanafunzi wa kada ya habari na wadau wa tasnia hiyo.



Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja, Othman Ali Maulid (wa tatu kushoto), akishirikiana na wananchi, kufanya usafi ufukweni mwa Bahari ya Hindi, katika Kisiwa cha Kwale, juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waonywa kugeuza maeneo ya Bahari majaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JAMII imetakiwa kutogeuza maeneo ya bahari kuwa majaa ya kutupia taka ili yaendelee kuwa na mazingira safi na kivutio cha utalii.

Akishiriki katika kusafisha fukwe kisiwani Kwale katika Hifadhi ya Menai, Wilaya ya Magharibi B Unguja, ikiwa sehemu ya Maadhimisho ya Siku ya Mvuvi Duniani, Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja, Othman Ali Maulid, alisema bahari na fukwe za Zanzibar ni miongoni mwa tunu zinazowavutia watalii kuvitembelea visiwa hivyo na kuinua pato la taifa.

Kutokana na hali hiyo, alisema wananchi wanaopaswa kujenga utamaduni wa kukusanya taka na kuzitupa katika maeneo maalum yaliyotengwa badala ya kuzimwaga fukweni na kuchafua mazingira ya Bahari. Alisema hali hiyo inaweza kuwakimbiza watalii.

"Sote tunajua umuhimu wa utalii ambao unachangia asilimia 30 ya pato la taifa. Uchafu si mzuri kama ambavyo sisi hatuupendi na watalii ndiyo zaidi. Ufike wakati tuuchukie kwa vitendo ili nchi ipendeze na kuendelea kuwa kivutio kwa wageni," alifafanua.

Mameneja wa Hifadhi za Bahari, walisema kuweka safi mazingira ya fukwe ni kutekeleza pia sera ya uchumi wa buluu ambayo kwa kiasi kikubwa inahusisha bahari.

Dk. Thani Rashid Said, Meneja wa Hifadhi ya Menai, alisema katika bahari kuna rasilimali nyingi wakiwamo viumbe hai mbalimbali ambao ili waishi na kustawi vizuri, ni lazima jamii iendeleze usafi katika maeneo hayo na kuondosha taka zote zinazoathiri viumbe.

Sambamba na hayo, aliwashauri wavuvi kutumia nyenzo zinazoruhusiwa kisheria ili kuepusha uharibifu wa matumbawe na majani bahari yanayotegemewa sana na viumbe.

Aidha, aliwasihi wananchi kuacha kukata miti ovyo ili kuifanya bahari iwe na afya bora hivyo kusaidia kuimarika kwa uchumi wao na nchi kwa jumla.

Meneja huyo alivipongeza vikundi mbalimbali vilivyoshiriki kuunga mkono zoezi hilo kama inavyohimizwa na viongozi wakuu taifa katika jitihada zao za kuimarisha uchumi wa buluu.

Wadau wa utalii kutoka mashirika mbalimbali, walisema usafishaji mazingira ya bahari na rasilimali zake unapaswa kuwa endelevu kwa manufaa ya jamii na taifa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI NOVEMBA 30, 2024



PHYNA KIVAZI CHAMPONZA Uk.14



## FEDHA ZIMESHINDWA

# Diddy kuendelea kusota rumande

KIBURI cha kuwa na pesa na umaarufu aliokuwa nao mwanamuziki wa Marekani, Sean "Diddy" Combs, kimefikia mwisho baada harakati za kujinasua kutoka mahabusu kushindikana.

Ni mara ya tatu sasa Diddy amekosa dhamana baada ya mahakama kukataa kutoka ndani, licha ya kutoa ofa ya kiwango kikubwa cha fedha.

Hakimu wa mahakama ya jiji la New York, amegoma kumpatia dhamana rapa huyo ambaye anaandamwa na utitiri wa kesi za unyanyasaji wa kingono na biashara ya dawa za kulevya.

Hapo awali, majaji wawili walikataa kuachiliwa Diddy, kutoka kizuizini, kwa sababu ya wasiwasi kuhusu uwezekano wa kuchezea mashahidi.

Waliona kuwa ni hatari ikiwa ataachiliwa kabla ya kesi, ambayo imepangwa kusikilizwa Mei 2025.

Diddy anazuiliwa katika gereza la Metropolitan, lililoko Brooklyn, jijini New York.

Hakimu alitoa ushahidi katika kesi hiyo unaoonesha madai ya mshtakiwa kuingilia ushahidi, ukiukaji wake wa kanuni za gereza akiwa gerezani na madai kwamba aliendesha biashara ya uhalifu pamoja na kazi ya kulazimishwa na utekaji nyara.

Jaji wa Wilaya ya Marekani, Arun Subramanian, alihitimisha kueleza kuwa mahakama haiwezi kumwamini Diddy ikiwa angeachiliwa kwa dhamana.

"Mahakama inaona kwamba serikali imeonesha kwa ushahidi wa wazi na wa kuridhisha kwamba hakuna masharti au mchanganyiko wa masharti yatahakikisha usalama wa jamii," jaji huyo aliandika katika uamuzi wake.

BASI SAWA



## Precious ataja siri ya ushindi

MREMBO Precious Epiphany, ambaye hivi karibuni ameshinda taji la Miss Polo, amesema kujiamini na kujikubali kama Mtanzania ndio siri ya mafanikio yake.

Amesema ushindi wake haukuwa rahisi kwani alishindana na washiriki kutoka mataifa 25 duniani kote na wote walihitaji kubeba taji hilo.

"Tunatakiwa kujikubali na kujiamini, hii ilikuwa ndio dira yangu nilipokuwa kwenye mashindano. Nawaomba Watanzania wenzangu waniunge mkono na tuendelee kuitangaza nchi pale tunapopata nafasi," amesema Precious.


## Idriss Sultan katoa ushauri wake



MWIGIZAJI staa, Idriss Sulatan, amesema katika maisha lazima kuwe na mipango zaidi ya mmoja kwa ajili ya kupambania mafanikio.

Amesema utaratibu huo unalazimisha watu kuwa na mbadala wa kupiga hatua, kutoka mpango mmoja hadi mwingine pale unaposhindwa kuona mwanga wa kutokea.

"Sikubaliani kuwa na mpango A na B katika maisha, kwangu mimi naamini kuwa na zaidi ya hapo hadi F kwani ukikwama unachukua mwingine ili kufika pale unapotaka," amesema Sultan.




## Paula ana vipaumbele vyake

PAULA Kajala ambaye kwa sasa anatoka kimapenzi na mwanamuziki maarufu, Marioo, ameonyesha ramani ya maisha yake ya baadaye, akisema elimu na ndoa ndiyo vipaumbele vyake.

Akizungumza hivi karibuni, mrembo huyo mama wa mtoto mmoja, amesema kutokana na kukatisha elimu anapenda kuendelea, lakini kwanza atimize ndoto yake ya kupata mume halali.

"Napenda sana kusomea mambo ya mitindo, lakini nitakwenda shule kama nitaolewa kwanza, hilo kwangu ni jambo muhimu katika maisha yangu," am.



## Vita ya familia haponi mtu

Na Adam Fungamwango

VITA ya familia ni filamu ya aina yake inayoonesha kuwa wakati mwingine ugomvi wa familia huanzia mbali. Unaweza kuona ukoo mmoja na mwingine unagombana, lakini tatizo lilianzia mbali na si kwa hao wanaogombana. Wakati mwingine inakuwa ni kulipiziana kisasi kwa ugomvi uliotokea kizazi kilichopita, au hata vizazi viwili au vitatu kutoka hapo.

Mtunzi wa filamu hii, alitaka kuikumbusha jamii kuwa wanapoona familia au ukoo unagombana na wanapotaka kusuluhisha, basi waanzie nyuma ili kugundua chanzo cha tatizo, badala ya kukurupuka.

Imechezwa na wasanii Salum Hamisi, Jackson Mayunga, Aisha Rajab, Angel Nicolaus, Karim Kitwana, Mariam Idd, Mary Damas na wengineo.

Inaanza kumwonesha Mayunga akiwa nje ya nyumba yao. Lakini anapita mtu mmoja anayeonekana kama kichaa na kumwomba chakula.

Mayunga anampa chakula. Akagundua kuwa mtu yule si kichaa, ila maisha magumu ndiyo yamesababisha vile. Hata anavyoongea ilionekana ni kijana mwenye akili zake.

Mayunga anaanza kumwamini kijana yule aliyeitwa Karim na kumshirikisha kwenye ushauri wa mambo ya kifamilia.

Mayunga ni mtoto wa mke mdogo kwenye familia hiyo. Hata hivyo baba na mama yake walishafariki, hivyo analelewa na mke mkubwa.

Mke mkubwa yeye alikuwa na watoto Salum Aisha na Mamu. Mke mkubwa alijitahidi kuwalea kwa uzazi sawa, lakini kwa Mayunga aliona kama anaonewa.

Akaenda kwa mganga ili amuue mama yake mkubwa, halafu baadaye anamuue Salum ili yeye awe mtawala wa nyumba ile.

Anafanikiwa kumuua mama yake mkubwa. Hata hivyo, tuhuma zinamwangukia Salum ambaye yeye alikutwa chooni alikokwenda kwa jitihada za kutaka kumwokoa mama yake mzazi, ikashindikana. Kila mmoja akadhani yeye ni muuaji. Akatoroka. Aliporejea akawa taahira. Polisi wakakataa kumkamata.

Mayunga tayari nyumba alikuwa ameishika. Ameitawala. Wote ameshawaweza. Amebaki na kinadada tu.

Siku moja analetewa barua. Anaisoma machozi yanaanza kumtoka. Kumbe alidanganywa na yule kijana Karim ambaye alimtumia tu ili amuue yule mama kwa sababu ana kisasi naye.

Kisa ni kwamba, mama yule aitwaye Zubeda ndiye aliyesababisha mama yake Karim aachwe na kuolewa yeye, baada ya wote kupewa mimba na mwalimu mmoja ambaye ndiye baba yao kina Mayunga.





## Rosa Ree anapenda wazee

RAPA anayependwa zaidi, Rosa Ree, amesema katika uhusiano wake wa kimapenzi hataki kujihusisha na wanaume vijana na wenye hekaheka nyingi.

Amesema katika maisha yake anapenda mwanaume aliyetulia na mwenye mawazo ya kiutu uzima ambaye anaweza kumshauri na kumwongoza katika shughuli zake.

"Mimi nawapenda wababa, sipendi wanaume ambao hawajatulia na wenye hekaheka nyingi. Mimi ni mtu ninayependa kutulia kimapenzi siwezi kujichanganya na mwanaume anayependa kuwa na wanawake wengi," amesema Rosa Ree.

## Povu la Ma-ex balaa

Na Adam Fungamwango

KWA hali ya kawaida ya binadamu, kuachwa na mpenzi ni jambo baya sana ambalo hataki limtokee.

Mtu anapokuwa na mpenzi na wanapendana, anaona kama dunia yote ni ya kwake. Anatamani aote mabawa aruke juu na kuiambia dunia nzima jinsi gani anapendwa.

Hali inakuwa tofauti sana pale wanapoachana. Na hata mmoja anapoachwa. Unaweza kuomba ardhi ipasuke ili uingie. Mtu anayeachwa anaweza kuona kama dunia yote inamwonea. Ataomboleza na kuongea yote. Wanamuziki na wasanii wanalijua hili. Ni watu anaoishi kwenye jamii na ama yamewakuta au wameyaona. Leo tuna nyimbo zinazowahusu watu walioachwa na wapenzi wao.

**Kuachwa-Khalid Chokoraa**

Wimbo huu ulitoka katikati ya miaka ya 2000, utunzi wake Khalid Chokoraa. Unazungumzia jinsi mtu aliyeachwa anavyojisikia vibaya. Mbaya zaidi ni kuona mpenzi wake aliyemwacha ananenepa, halafu yeye anakonda kwa mawazo. Ni moja kati ya vitu vibaya na usiombe yakukute.

**Mama Rhoda-Jose Chameleone**

Mwanzoni mwa miaka ya 2000, msanii kutoka Uganda, Jose Chameleone, alitoka na wimbo unaosema 'Mama Rhoda'.

Mtunzi anamlalamikia mama Rhoda kwa nini amemwacha na anamwambia kuwa ipo siku atamkumbuka. Ni kwamba mama Rhoda amemkimbia na kumuacha na watoto.

**Shahada ya uvumilivu-DDC Mlimani Park**

Ni wimbo wa masikitiko sana. Ulitungwa katikati ya mwishoni mwa miaka ya 1980. Ni stori ya mtu anayetunukiwa shahada ya uvumilivu na rafiki zake. Ni baada ya kukimbiwa na mkewe ambaye alirubuniwa na mwanaume kwa ahadi ya pesa na kujengewa nyumba. Jamaa ilimuuma sana, lakini hakulipiza kisasi cha hasidi aliyemrubuni mkewe. Badala yake aliacha kama ilivyo, lakini akiugulia maumivu moyoni.

**Tuma-Juwata Jazz Band**

Katikati ya miaka ya 1980, Tx Moshi William alitunga wimbo wa 'Tuma', unaomzungumzia mtu aliyesimama kwenye kona ya barabara za Uhuru na Msimbazi akitazama wanaokwenda na kurudi kama anaweza kumuona mpenzi wake Tuma walioahidiana kupelekana kwa wazazi.

Jua liliwaka, hadi lilizama, demu hakuonekana. Jamaa alikuwa ameachwa kwenye mataa.

Kwa huzuni, jamaa anaombolewa kuwa ni matatizo kumpenda mwanamke mrembo anayependwa na wengi, unaweza kunywa sumu au kujinyonga. Hata hivyo kwa kuwa yeye ni kijana, basi atasonga mbele na maisha mengine.

**Mchumba Hanitaki-Simba Wanyika**

Ilikuwa ni mwishoni mwa miaka ya 1970, Willson Peter alipotunga wimbo wa 'Mchumba Hanitaki.'

Jamaa analalamika kuwa mchumba wake awali alikuwa anampenda na walipanga kuoana, lakini kwa sababu sasa pesa na kazi hana, amemua kumsaliti na kumkataa mchana kweupe.

Jamaa analalamika alie na nani.



CHAMELEONE




# Wizkid amjibu kiutuuzima Davido

STAA wa muziki wa Afrobeats kutoka Nigeria, Wizkid, ameonyesha yuko makini na kazi, wakati mpinzani wake Davido, akiegemea siasa za nchi hiyo.

Jana, Wizkid ameweka video fupi katika ukurasa wake wa Instagram, akionekana akitoa burudani jukwaani katika tamasha moja katika nchi za Ulaya.

Video hiyo inaonekana kama jibu kwa Davido ambaye hivi karibuni alisikika akiisema vibaya nchi yake kuwa hali ya kiuchumi inazidi kuwa mbaya.



## Sypro roho yake safi

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Oludipe Oluwasanmi David, maarufu Spyro ameelezea wasiwasi wake kuhusu watu wanaodai halipo watu wanaoshiriki kuandaa muziki wake.

Spyro, amesema anatoa pesa za kutosha lakini bado wnaichagua kucheza na kili za watu kwa kueneza hisia hasi kwake.

Amesema kutokana na imani yake ya Kikristo anaamini watu hukosea na kudanganya na hivyo ni wajibu wake kuwasamehe.

Kama mtu anayeweza kudanganywa, na chapisho lake liliwafanya watumiaji wa mitandao kuguswa na mwimbaji wa Nigeria Oludipe Oluwasanmi David, almaarufu Spyro, amefunguka kuhusu baadhi ya wenzake walikuwa na deni lake na waliamua kufanya kama si kitu.

## Speed Darlington adakwa

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Darlington Okoye, maarufu kama Speed Darlington, amekamatwa na polisi baada ya kumhusisha msanii mwenzake Burna Boy, na rapa wa Marekani Diddy.

Wakili Deji Adeyanju, Jumatano, aliandika kwenye ukurasa wake wa X, aliwafahamisha wafuasi wa mwanamuziki huyo kuwa alikamatwa na polisi wa jimbo la Imo.

Kukamatwa kwake kunazidisha uvumi kwamba wasanii hao hawajamaliza ugomvi wao, licha ya awali kuonekana wameweka tofauti zao pembeni kwa manufaa ya muziki wao.





## Falz kumbe alihonga chakula

RAPA wa Nigeria, Falz amefunguka kuhusu tukio lake la kwanza la kuwanunulia wakwe zake chakula.

Akizungumza hivi karibuni, Falz amesema hakuwa na uzoefu kuhusu wanawake, lakini siku hiyo mrembo aliyekuwa akimpenda alimtaka aende kuwanunulia wanafamilia wake chakula na awapelekee nyumbani.

"Sijapata uzoefu mwingi suala la kuchumbiana lakini mbaya zaidi pengine ni msichana yule alikuwa ananijaribu, aliniomba kununua vitu kwa ajili ya familia yake nyumbani," amesema.

## Phyna kivazi champonza

ALIYEKUWA mshiriki wa shindano la Big Brother Nigeria, Phyna, amekataliwa kuingia katika mgahawa baada ya kuvaa mavazi yenye utata.

Mmiliki wa mgahawa huo unaoitwa Cali ulioko katika jiji la Logos nchini Nigeria, alikataa msanii huyo kuingia ndani kupata chakula kutokana na mavazi yake kuwa kinyume na maadili.

"Nilienda kula chakula cha jioni kwenye mgahawa wa CALI kama wanavyoita mahali hapo, waliniambia siwezi kuingia kwa sababu nimevaa nguo isiyo na heshima," amesema Phyna.



# Mipango yaandaliwa kukabili upungufu maji

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

SERIKALI imepanga kuanza kutekeleza miradi mipya 32 ya ukarabati, ukaguzi, utafiti na uchimbaji wa visima virefu vya maji katika mkoa wa Manyara, ili kukabiliana na makali ya mgawo wa maji unaotokana na vyanzo vichache vya maji.

Miradi hiyo itatekelezwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25, ikiwa na thamani ya Sh. bilioni 77.3.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Manyara, James Kionaumela, alisema mpango huo unatokana na wastani wa uzalishaji wa maji kwenye skimu 209 za mkoa huo, kuzalishwa lita 42,000.7 kwa siku.

"Kwa sasa kuna miradi 22 yenye thamani ya Sh. bilioni 90.9 inaendelea na utekelezaji na miradi 32 mipya ya ukarabati, ukaguzi, utafiti na uchimbaji wa visima kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25 yenye thamani ya shilingi bilioni 77.3, ndio inategemea kuanza kujengwa mwaka huu," alisema.

Meneja huyo alisema kati ya vijiji 440 vya Mkoa huo, RUWASA inahudumia vijiji 396, ambapo kati ya vivyo, vijiji 277 vina maji ya mtandao na vijiji 52 vinatumia pampu za mkono na umeme wa jua (sola).

Vilevile, alisema upatikanaji wa maji vijijini ni asilimia 75 na wakazi wanaohudumiwa ni mil. 1.5, ambapo wenye maji ni wananchi milioni 1.06.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, alisema kwa mwaka wa fedha 2023/24 mkoa umepokea Sh. bilioni 190 kutekeleza miradi ya maendeleo ya sekta mbalimbali zikiwamo maji, afya, elimu, utawala, uwekezaji, biashara, kilimo na nishati. Sendiga alisema kwa sekta ya elimu imejengwa shule ya sayansi ya wasichana na shule ya wavulana inajengwa hadi Desemba itakamilika.

Pia alisema shule za msingi madarasa 249 yamejengwa, matundu ya vyoo 389 yamejengwa na maabara 14.

Kuhusu afya alisema zimejengwa zahanati 19, vituo vya afya 11, ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali mbili za wilaya.



Mdau wa Maendeleo, Enock Koola (kushoto), akikabidhi cheti cha heshima kwa mwanafunzi bora wa masomo, Solomon Nnko, wakati wa mahafali ya 28 ya kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Acape Seminari, wilayani Moshi, mkoani Kilimanjaro hivi karibuni. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# Wachangamkia kilimo cha matunda

**Na Godfrey Mushi,** HAI

TIJA kubwa ya kipato katika uzalishaji wa mazao ya matunda ya strawberry, vanila na parachichi, umeivutia Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, kujikita kuyalima kama mazao mbadala ya kiuchumi kwa wananchi wake.

Akizungumzia uamuzi huo jana, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Edmund Rutaraka, alisema kwa mfano zao la strawberry, hukua vizuri katika mwinuko wa mita 1,500 na zaidi kutoka usawa wa bahari na kwa Tanzania lina uwezo wa kustawi zaidi katika mikoa kama Morogoro, Mbeya, Iringa, Arusha na Kilimanjaro.

"Tumeamua kwamba, kwa vile strawberry hustawi katika maeneo yenye joto la wastani, na hukua kwa haraka zaidi na uzalishaji kuongezeka linapolimwa kisasa zaidi, hasa katika green house (shamba kitalu), tuwahamasishe wananchi wetu kuwekeza katika kilimo hiki," alisema.

Kuhusu parachichi, alisema hivi sasa wanawasiliana na mwekezaji aliyepewa zabuni ya ujenzi wa kiwanda cha kuchakata zao hilo, ili kuongeza fursa za kiuchumi kwa wakulima, ambao kwa sasa wamekuwa wakitegemea wanunuzi binafsi, huku baadhi wakilalamikia bei kuyumba.

Rutaraka, amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji, Dionis Myinga, Ofisa Ushirika na Mwanasheria, kwenda kumkumbusha mwekezaji juu ya mkataba wake na kumsukuma kuanza utekelezaji.

Mbunge wa Hai (CCM), Saashisha Mafuwe, alisema: "Sasa hivi tunatafuta namna ya kufanya kuimarisha na kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja, ndio maana tukaja a uwekezaji kwenye zao la parachichi.

"Chama cha Ushirika cha MROSOSANGU, kilitia mkataba na mwekezaji huyo na kusimamiwa na Mrajisi wa Vyama vya Ushirika nchini.

"Kwenye mkataba ule kwenye Chama cha MROSOSANGU, ambako tumempata mwekezaji James (mzungu), tulikubaliana kabla ya mwaka 2025 awe ameanza kujenga kiwanda cha parachichi. Kiwanda ambacho kitachukua parachichi za kisasa na ile reject kwa ajili ya kutengeneza mafuta," alisema.

Kwa mujibu wa Saashisha, ametembelea na kukagua eneo hilo lakini mpaka sasa mwekezaji hajaanza kazi hiyo.

Ofisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai, Zephania Gunda, alisema azimio la kwanza la Baraza la madiwani, linahusu wakulima ambao wanamiliki maeneo ya kilimo, hasa ukanda wa kati na ukanda wa juu, washauriwe kutenga maeneo na kuanza kilimo cha parachichi, kwa hali ya hewa ni rafiki wa parachichi na soko lake ni kubwa, na hasa kwa uzalishaji unaofanyika cha kiangazi kwa njia ya umwagiliaji.

Azimio la pili, ni kwa wakulima wenye uwezo washauriwe kujenga viwanda vya kusindika parachichi, kwa kuwa tayari baadhi ya wakulima wanazalisha parachichi katika halmashauri yetu na ukanda wa kaskazini, na kunawalazimu wanunuzi kupeleka kwenye viwanda nje ya nchi kwa ajili ya usindikaji, kwa kuwa Tanzania hatuna viwanda vya usindikaji.

Tayari, China imefungua soko jipya la parachichi zinazozalishwa Tanzania, baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kutia sahihi mkataba wa mauzo ya zao hilo na serikali ya nchi hiyo.

Soko hilo litaongeza kiwango cha parachichi kinachouzwa nje ya nchi kwa sasa kutoka tani 12,000 za sasa hadi kufikia tani 10,000.

## Samia kufungua mkutano majaji Afrika Mashariki

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ZAIDI ya majaji na mahakimu 390 wanatarajia kushiriki katika kongamano na mkutano mkuu wa 21 wa Chama cha Majaji na Mahakimu wa Afrika Mashariki (EAMJA), utakaofanyika Desemba 2 hadi 7, mwaka huu, jijini hapa.

Ufunguzi wa mkutano huo utafanyika Desemba 3, mwaka huu na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

Jaji wa Mahakama ya Rufani, Dk. Gerald Ndika, ambaye ni mwenyekiti wa maandalizi ya kongamano na mkutano huo, alitoa taarifa hiyo jana jijini hapa.

Alisema chama hicho, kilianzishwa mwaka 2000 na kuzinduliwa Uganda mwaka 2001 na hadi sasa kimetimiza miaka 24 tangu kuanzishwa kwake.

Alisema lengo la chama hicho ni kutoa jukwaa kwa wahusika kukutana na kujadiliana namna bora ya kuboresha utendaji kazi wao, kupeana uzoefu na kujadiliana kuhusiana na changamoto na mafanikio waliyopata.

Pia alisema lengo lingine la chama ni kutetea na kulinda uhuru wa Mahakama kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) pamoja na kuhakikisha nchi hizo zinakuwa na utawala bora wa sheria.

"Nchi yoyote ile haiwezi kuwa na maendeleo bora ikiwa na changamoto za utawala wa sheria na mfumo wa utoaji wa haki, hivyo jukwaa hili linawawezesha majaji na mahakimu kukutana na kubadilishana uzoefu," alisema Jaji Ndika. Alisema nchi ambazo zimethibitisha kushiriki mkutano huo ni Tanzania Bara, Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi, Sudani Kusini na Zanzibari huku Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Somalia zikiwa bado hawajathibitisha. "Maudhui ya mkutano tutaangalia uboreshaji wa mifumo ya utoaji haki kwa ajili ya kuimarisha utangamano na ukuzaji uchumi katika ukanda wa EAC, pia tutaangalia uboreshaji wa mifumo ya utoaji haki," alisema.


Pia alisema katika kongamano na mkutano huo, utawawezesha kujadiliana na kupitia maeneo mengine mahususi matano ambayo ni kuangalia utendaji kazi katika eneo la utoaji haki kwa haraka zaidi.


Alisema eneo lingine, litakuwa kuangalia programu za maboresho ya mifumo ya utoaji haki jinai, programu za maboresho ya mfumo wa utoaji haki katika mashauri ya madai, uboreshaji utoaji haki kwenye migogoro ya kazi, matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) na uimarishaji wa utoaji wa maamuzi kuhusiana na mashauri ya makosa ya jinai na uhamishaji wa fedha unaovuka mipaka.

## TULIKOTOKA,TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Wapenzi walivyopatikana kuwasiliana bila simu, meseji, mitandao, enzi hizo

**Na Adam Fungamwango**





TEKNOLOJIA kwa kiasi kikubwa imebadili baadhi ya utamaduni na mfumo wa maisha ya zamani. Leo tutazungumzia zaidi teknolojia ya simu za mkononi ambazo zimeleta utamaduni, na utaratibu mpya kabisa za maisha, tofauti na ule wa zamani. Mwingine ni hasi na mwingine ni chanya.

Kumbuka simu za mkononi zilianza kuwepo nchini katikati ya miaka ya 1990, tena zilikuwa chache na wamiliki wake pia, huku ikiwa ni gharama kubwa kuimiliki. Kwanza zilikuwa kubwa kama 'radio call', halafu kula teknolojia ilivyozidi kukua, zikawa zinapungua uzito na ukubwa pia.

Angalau watu wengi walianza kumiliki simu kuanzia miaka ya 2000 na kuanzia hapo simu ikawa si anasa tena, bali ni maisha. Baadhi ya watu bila simu sasa hawezi kufanya kitu chochote kile. Hawezi hata kuingiza pesa. Kula yake na kuvaa inategemea simu ya mkononi.

Kipo kizazi ambacho kimeondoka duniani kikiwa hakijatumia kabisa simu za mkononi. Na kuna kizazi ambacho kama chaja ya kobe, chenyewe kimeishi maisha ya bila simu na pia wakati huu wa maisha ya simu za mkononi. Sasa kuna kizazi cha sasa ambacho chenyewe kimezaliwa kimezikuta simu za mkononi kwa wingi.

Hawa wakisimuliwa maisha ya watu waliokuwa wanaishi bila simu wanashangaa. Wanaona kama ni hadithi za kufikirika hivi. Na wanaoamini wanaona kama kizazi hicho kilipata shida sana. Wakati mwingine wanaona kama ni burudani hivi kwa jinsi shida zilivyokuwa zikiwapata baba na kaka zao.

Usiombee sasa ukutane na kizazi ambacho kimeishi maisha yote ya pande mbili. Wao wanapokaa na kuhadhithiana jinsi walivyofanya, staili walizotumia na vituko mbalimbali, inakuwa ni burudani iliyotikisa.

Mume akitaka kumsafirisha mke, mfano kwenda kwao kusalimia, basi ilikuwa ni lazima ampe nauli ya kwenda, kurudi na ya matumizi ya njiani. Asipofanya hivyo hawezi kurudi, mpaka atume nauli kwa njia ya posta na ilichukua muda mrefu kufika kwa uchache wiki tatu hivi au zaidi, tena ipitie kwa mtu mwenye sanduku la posta. Na akiondoka hawawezi kuwasiliana tena hadi arudi, au yoyote kati yao aandike barua na kuituma posta.

Kwa sasa mume anaweza kumpa nauli tu mke ya kwenda. Halafu wakawa wanawasiliana kama vile wako wote kila simu au kila muda watakaopenda kupigiana simu au meseji. Na mke akitaka kurejea anamwambia tu mumewe, pesa itatumwa kwenye simu siku ile ile ya kurudi na nauli itapatikana na tiketi itakatwa. Wanaweza hata kuwasiliana "umefika wapi?" Hiyo ndiyo teknolojia.

Kutokana na kukua kwa teknolojia, imerahisisha hata jinsi ya wanaume au vijana wa sasa kupata wenza wao, ambao mwanzo wanakuwa wapenzi, baadaye wachumba na mwisho wanakuwa wake zao.

Kijana wa sasa hana mambo mengi. Ataomba namba ya simu tu ya msichana, biashara imekwisha, mambo mengine yataenda taratibu hadi yatakaa yenyewe sawa. watawasiliana na kubembelezana kila siku. Iwe kupigiana simu, meseji, na kwa sasa kuna simu janja, basi hata 'WhatsApp', na mitandao mabalimbali ya kijamii kama facebook, Instagram na mengine, mambo yasipokaa sawa, basi siyo bahati yako.

Imerahisisha hata jinsi ya kukutana. Yoyote yule anapiga simu kuwa wakutane sehemu fulani, kituo fulani ana maeneo fulani. Mwingine hata kama amefika, lakini atampigia mwenzake kujua amekaa wapi,"uko wapi?", "mbona sikuoni?" "Aah basi nimekuona." Ni rahisi sana tofauti na zamani. Sasa hebu sikiliza masahibu waliyokuwa yakiwapata vijana, au wanaume wa zamani.

Hakuna namba za simu au simu zenyewe, hivyo anapokutana na msichana ni lazima amkabili uso kwa uso na kumwambia ukweli kuwa anampenda, vinginevyo imekuwa kwake.

Kuna wakati inashindikana kutokana na mazingira au kuona aibu, hivyo kulikuwa na njia mbadala ambayo ilikuwa ni ya hatari, kuandika barua na kumpa rafiki yake ampelekee au kumtuma mtoto.

Hii wakati mwingine ilinajulikana kwa wazazi na walimu, pale barua itakaangukia mikononi mwa wasiohusika kwa bahati mbaya.

Na hata ahadi za kukutana zilifanyika pale wanapokuutana wawili. Watapanga kukutana lini na staili fulani ya kufanya ambayo ni wao tu ndiyo wataifahamu. Ni kwamba kijana atapiga nyumbani kwa msichana na kurusha kijiwe juu ya bati ili iwe wito kuwa anapita sasa na yeye atoke. Wakati mwingine mwanaume anapiga hata miluzi au kuimba. Anayejua nini kinatakiwa kufanyika ni msichana tu.

Kuna kuahidiana kukutana siku fulani, sehemu fulani, na saa fulani. Sasa kama msichana hakufika siku hiyo basi hiyo ndiyo inaitwa 'kuachwa solemba'. Ni tofauti na sasa, kabla yoyote hajanyanyua mguu, kama kuna dharura watajulishana "siwezi kuja leo, shangazi anaumwa." Ni faida kwa vijana wa sasa kabla ya kuelekea kwenye ahadi. Wale wa zamani walikuwa hawana faida hiyo, atafika na atapoteza muda na gharama kama msichana hakuja. Hii ni kutokana na kutokuwa na teknolojia ya simu.

Kuna waliokuwa wakishindishwa kwenye vibaraza, chini ya mti, kwenye kona za nyumba za watu na sehemu zingine zinazofanana na hizo. Kuna wengine waliwahi kufurumushwa na nyuki, nyoka, mbwa kutambaliwa na washawasha, kuumwa na nyigu wakiwasubiri wapenzi wao, hasa wale wa vijijini. Kumbuka hizi zote ni zile hatua ya mwanzo kabisa, kabla ya kijana kwenda kujitambulisha kwa wazazi.

Vijana wa zamani wanasema kuwa ugumu waliokuwa wakiupata wao ndiyo unasababisa hata ndoa zao kudumu, kwa sababu waliwapata wapenzi, wachumba na wake zao kwa tabu. Kwa njia ngumu na za hatari, zilizohitaji uvumilivu wa hali juu, tofauti na vijana wa sasa ambao wanawapata kirahisi, kwa kurahisiwa kazi na teknolojia ya simu za mkononi.

Sijui kama kuna ukweli au la, lakini ukweli inabaki pale pale kuwa kabla ya teknolojia ya simu za mkononi, aliyekuwa anatafuta msichana ilibidi aache kazi afanye kazi. Yoyote atakayekusimulia jinsi alivyompata mkewe ni zaidi ya burudani, unaweza kukauka au kuvunjika mbavu kwa kucheka, kwani kila mmoja alikuwa na staili yake, zinazovutia kuzisikiliza.

**Tuma meseji 0716 350534**

HABARI KIMATAIFA

# Chad yasitisha uhusiano wa kijeshi na Ufaransa

**N'DJAMENA,** CHAD

CHAD imesitisha makubaliano ya ushirikiano wa kiulinzi na Ufaransa, na kuibua wasiwasi wa kupungua kwa ushawishi wa nchi hiyo iliyokuwa koloni lake.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Chad, Abderaman Koulamallah, alisema ni wakati wa nchi yake kudai mamlaka yake kamili.

Tangazo hilo limekuja saa chache baada ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Ufaransa, Jean-Noel Barrot, kukutana na Rais wa Chad Mahamat Deby.

Chad ni mshirika mkuu katika mapambano ya nchi za Magharibi dhidi ya wanamgambo wa Kijihadi katika eneo la Sahel katika eneo la Afrika Magharibi.

Lakini kabla ya uchaguzi wa rais mwezi Mei, mamlaka ya Chad iliamuru kuondolewa kwa wanajeshi wa Marekani nchini humo, kuashiria kujitenga na washirika wa jadi wa nchi hiyo.

Ufaransa kwa sasa ina wanajeshi 1,000 katika nchi hiyo ya Afrika ya Kati ambao wanatoa usaidizi wa kijasusi na vifaa kwa wanajeshi wa Chad kutoka katika kambi zao, ukiwamo katika mji mkuu N'Djamena.

Ufaransa, mtawala wa zamani wa kikoloni wa Chad, ilitia saini toleo lililorekebishwa la makubaliano ya kijeshi na usalama mnamo 2019.

**BBC**



Wananchi wakisaidia uokoaji wa watu walionaswa kwenye udongo baada ya kutokea maporomoko ya ardhi katika kijiji cha Bulambuli, Uganda. **PICHA: AP**

# Utulivu unazidi kuimarika Lebanon

**BEIRUT,** LEBANON

ISRAEL imesema vikosi vyake vya kijeshi vimefyatua risasi na kufanya mashambulizi ya anga dhidi ya maeneo yaliyolengwa ya kusini mwa Lebanon.

Hatua hiyo imechukuliwa baada ya siku ya pili ya makubaliano ya usitishaji mapigano uliosimamiwa baada ya vita kati ya Israel na kundi la Hezbollah kuchukua zaidi ya mwaka mmoja.

Jeshi la Israel lilisema liliwafyatulia risasi washukiwa baada ya kuona shughuli katika kituo cha silaha cha Hezbollah, na magari yakiwasili katika maeneo kadhaa ambayo yalikiuka masharti ya makubaliano ya usitishaji wa mapigano.

Lebanon iliishutumu Israel kwa kukiuka makubaliano mara kadhaa na kusema inafuatilia hali hiyo.

Hadi jana usitishaji wa mapigano unaonekana kufanikiwa kwa kiasi kikubwa, na barabara ya kijeshi ya Israeli inayoelekea ncha ya kaskazini ya mpaka wa Lebanon ilikuwa tulivu kuliko ambavyo imekuwa kwa miezi iliyopita.

Kupitia lango hilo lililo wazi, ilishuhudiwa askari wakifanya matengenezo ya kawaida ya zana za kijeshi.

Nahodha mmoja, ambaye alivuka Lebanon asubuhi ya jana, alisema yeye na timu yake walikuwa na furaha kuondoka kwenye mapigano na kurejea katika maisha yao ya kawaida, lakini akisema anatumai pande zote zimetekeleza yanayohitajika.

"Lasivyo, sote tunaelewa kuwa tutajikuta tumerudi hapa hivi karibuni," alisema.

Aliongeza "Binafsi, nadhani bado kuna kazi ya kufanya. Ni wazi kwamba Hezbollah bado ina nguvu za kutosha kuitishia Israel."

Wakati huo huo, Jeshi la Israel limewaonya raia wa Lebanon kutorejea katika vijiji 60 kusini mwa nchi hiyo.

Maelfu ya watu walikuwa wakirejea katika makazi yao siku tatu baada ya kusitishwa kwa mapigano.

Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF) lilichapisha ramani inayoonyesha eneo lenye kina cha maili kadhaa, ambalo lilisema wakazi hawapaswi kurudi.

Lilisema, yeyote atakayefanya hivyo atakuwa anajiweka hatarini.

Zaidi ya Walebanon milioni moja wamekimbia makazi yao kutokana na mapigano hayo, wengi wao kutoka eneo la kusini.

Usitishaji wa mapigano ulianza kutekelezwa Jumatano asubuhi, ingawa maofisa wa Israel na Lebanon wameshtumiana kila mmoja kukiuka makubaliano.

Alhamisi jeshi lilisema vikosi vyake vilifyatua mizinga na kufanya mashambulizi ya anga dhidi ya wapiganaji wa Hezbollah kusini mwa Lebanon.

Lebanon iliishutumu Israel kwa kukiuka makubaliano mara kadhaa na kusema inafuatilia hali hiyo.

**BBC**

# Watu 113 bado hawajapatikana maporomoko ya ardhi Uganda

**KAMPALA,** UGANDA

ZAIDI ya watu 100 bado hawajulikani waliko kufuatia mkasa wa maporomoko ya ardhi yaliyotokea mashariki mwa Uganda.

Maiti ambazo ziliopolewa kwenye tope imefikia 18, huku miili ya watu wanne ilipatikana usiku wakuamkia jana.

Hata hivyo, hofu imetanda kutokana na idadi kubwa ya watu wanaofikia 113 hawajulikani waliko na wasiwasi wa wananchi vijiji vitano vilivyoathiriwa kuwa huenda wamefariki dunia.

Polisi ilithibitisha idadi hiyo ya watu ambao bado wanatafutwa ili kubaini hali yao.

Mwanahabari Gerald Matembo ambaye anafuatilia shughuli za uokozi akiwa eneo la tukio, aliambia Dw kuwa hali imekuwa ngumu kutokana na ukosefu wa vifaa vya kufukua kifusi cha udongo.

"Unadhani kuna hali gani ambayo vijiji vitano vimefunikwa na tope na watu zaidi ya mia moja hatujui kama watapatikana wakiwa hai au la," alisema.

Kulingana na msemaji wa Shirika la Msalaba Mwekundu, John Cliff Wamala, alisema shughuli ya uokoaji inaendelea, lakini ni watu 32 waliofanikiwa kuokolewa na kuwakimbiza kwenye vituo vya afya.

Alisema kinachosumbua ni hali ya hewa na ubovu wa barabara inayozuia kuwezesha vifaa muhimu kufikishwa kwenye vijiji hivyo vitano.

Wamala alifafanua kuwa kuhusu hali halisi ya maafa na hasara inaendelea kutathminiwa.

"Nyumba 45 zimefukiwa na tope na mali za watu ikiwamo mifugo na mashamba yameharibiwa. Tunaendelea na operesheni kwa kusaidiana na jeshi la polisi na wananchi." Alisema Wamala.

Watu kadhaa walionusurika walisimulia jinsi walivyotengana na jamaa zao na wanahimiza kuwepo juhudi za kuwapata wakiwa hai au wakiwa wamefariki ili wawafanyiwe maziko yanayostahiki.

**DW**

# Iran yataka Ulaya kubadili mtazamo

**TEHRAN,** IRAN

IRAN imetoa wito kwa Umoja wa Ulaya kubadili mwenendo wake kwa nchi hiyo, baada ya kufanya mazungumzo na mwanadiplomasia mkuu wa Umoja huo, Enrique Mora.

Katika taarifa iliyochapishwa katika mtandao wa kijamii wa X, baada ya ujumbe wa Iran kufanya mazungumzo na Mora, ukiongozwa na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Kazem Gharibabadi, alisema ilithibitishwa tena kwa Mora kwamba Umoja wa Ulaya unapaswa kuacha tabia yake aliyoitaja kuwa ya ubinafsi na kutowajibika kwa maswala na changamoto za bara hilo na mambo ya kimataifa.

# Serikali yatambua mchango wa sekta binafsi

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

SERIKALI imesema inatambua mchango wa sekta binafsi katika uwekezaji na imeendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara kupitia utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara.

Kamishna Msaidizi Idara ya Sera anayeshughulikia masuala ya Ushirikiano wa Kimataifa katika Masuala ya Kodi na Mwenyekiti wa Kongamano la Kodi, Juma Mkabakuli, aliyasema hayo jana wakati wa Kongamano la Kodi lililofanyika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, mkoani hapa.

Mkabakuli alisema, ili sekta binafsi ishiriki kikamilifu katika kukuza uchumi wa nchi, serikali inaendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini na imefuta na kupunguza baadhi ya ada na tozo kero takriban 379.

Alisema, serikali inaendelea kuhakikisha uhimilivu wa viashiria vya uchumi jumla; kuwa na sera za kodi zinazotabirika na kuwianisha tozo na ada mbalimbali zinazotozwa na wizara na mamlaka za udhibiti kwa lengo la kupunguza na kurahisisha ulipaji wake kupitia namba ya malipo jumuishi.

Mwenyekiti wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA) Mkoa wa Mbeya, Erick Sichinga, alisema wanaishukuru serikali kupitia Wizara ya Fedha kwa kuona umuhimu wa kuwa na majukwaa hayo kila mwaka kujadili sera za kodi.

"Mbeya tumebahatika kuwa moja kati ya mikoa ambayo makongamano haya yanafanyika. Nikilinganisha na kongamano ambalo lilifanyika mwaka jana na mwaka huu, nimeona kuwa kuna maendeleo makubwa ambayo sisi wadau wa sekta binafsi, tumeona serikali imeanza kuwa sikivu.

"Kero mbalimbali zimeanza kufanyiwa kazi, tumeona baadhi ya maofisa wakipita katika sekta binafsi kwa ajili ya kuchukua maoni na kuyafanyia kazi," alisema.

Sichinga alisema TCCIA inaendelea kufanya kazi kwa karibu na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na hivi karibuni wanatarajia kutia saini makubaliano ya utoaji elimu kwa mlipakodi kwa kuwa wanyabiashara wengi ni wadau wa TCCIA na lengo kuu ni kuboresha ulipaji kodi kwa hiari.

"Tunataka kuona TRA ni mlezi mkubwa wa biashara yako kwa hiyo kupitia session mbalimbali ambazo TCCIA tunazifanya wadau wetu wanapata elimu," alisema Sichinga.

Aidha, Sichinga alibainisha majukumu mbalimbali yanayofanywa na TCCIA yakiwamo kuratibu maonesho ya biashara kwa kuwakusanya wafanyabiashara na wazalishaji mbalimbali kwa ajili ya kuonesha bidhaa zao, kuandaa safari za kimsimu za wafanyabiashara, kutatua migogoro ya kibiashara.

Aliyataja malengo mengine kuwa ni kuwawezesha wafanyabiashara wanawake katika sekta ya ujasiriamali, kuibua wafanyabiashara wapya hasa vijana walioko vyuoni na waliomaliza vyuo pamoja na kuandaa mabaraza ya biashara kuanzia ngazi ya wilaya, mkoa na taifa.

Kongamano hili la Kodi Kanda ya Nyanda za Juu Kusini lilishirikisha wadau mbalimbali wakiwamo wafanyabiashara, wajasiriamali wadogo, sekta ya kilimo, biashara za usindikaji wa mazao na washauri wa kodi.

Wadau hao walitoa maoni mbalimbali na kuupongeza uongozi wa TRA Mkoa wa Mbeya kwa kuwa karibu na wafanyabiashara.



Mjasiriamali mdogo wa vyakula vya lishe, Sophia Mrwati, akichangia mada kuhusu ubora wa bidhaa, wakati wa Kongamano la Kodi Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mkoa wa Mbeya, juzi. **PICHA: WF**

# Madiwani wahimizwa makusanyo ya mapato

**Na Linah Rwambali,** SIKONGE

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge mkoani Tabora, Rashid Magope, ameitaka timu ya ukusanyaji mapato kushirikiana na madiwani ili kuwezesha ukusanyaji mapato kwa ufanisi.

Magope aliyasema hayo mapema wiki hii wakati akihitimisha kikao cha Baraza la Madiwani robo ya kwanza kilichofanyika katika ukumbi wa halmashauri mjini hapa.

"Madiwani mkahimize suala la mapato katika maeneo yenu ili kufikia lengo la makusanyo," alisema.

Aidha, Magope alisema kata 13 kati ya 20 zimefanya vizuri wakati zilizobaki hazikufikia asilimia ya lengo la makusanyo.

"Ninaiagiza timu ya kukusanya mapato iende katika hizo kata saba ambazo hazijafanya vizuri ili kubaini changamoto inayosababisha zinashindwa kukusanya mapato ipasavyo," alisema.

Sambamba na hilo, Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge itaongeza mashine 10 za ukusanyaji mapato kwa ajili ya ufanisi katika ukusanyaji mapato.

"Tumekubaliana tutanunua pos 10 mpya kwa ajili ya kuongeza mapato. Ninaamini pos (mashine za kukusanyia mapato) hizo 10 zitaenda kuongeza mapato katika maeneo yetu," alisema Magope.

Kwa mujibu wa Magope, kata sasa halmashauri hiyo imekusanya asilimia 23.34 ya lengo kwa robo ya kwanza, hatua ambayo ni nzuri kwa kuwa kuna vipindi vinne kwa mwaka.

**Tumekubaliana tutanunua pos 10 mpya kwa ajili ya kuongeza mapato. Ninaamini pos (mashine za kukusanyia mapato) hizo 10 zitaenda kuongeza mapato katika maeneo yetu.**

# Msisitizo wawekwa sekta ya mawasiliano ukuaji uchumi

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI imesema sekta ya mawasiliano imeendelea kuchangia pato la taifa na kukuza uchumi wa kidigital.

Waziri wa Habari na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa, kwenye uzinduzi wa jina jipya la kampuni ya Tigo Tanzania ambayo sasa inajulikana kama Yas Tanzania.

Silaa alisema Rais Samia Suluhu Hassan Julai, mwaka huu, alizindua mkakati wa miaka 10 wa uchumi wa kidigitali (2024-2033) na kampuni za simu zimekuwa washirika wakubwa kwenye mkakati huo.

"Serikali inatambua mchango wa makampuni ya simu katika kukuza uchumi wa nchi na kuchangia pato la taifa, tunaamini mabadiliko haya ya kampuni hii yataendelea kuchochea ukuaji wa kiuchumi," alisema Silaa.

Silaa pia alisema mpaka sasa matumizi ya huduma za fedha kwa njia ya simu yamefikia asilimia 60, hivyo kuonesha namna kampuni za simu zinavyoshiriki katika kukuza uchumi.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Zanzibar, Dk. Khalidy Salum Mohamed, alisema Serikali ya Zanzibar imeona juhudi za kuchochea uchumi zinazofanywa na kampuni za simu.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua umuhimu wa wawekezaji kwenye sekta ya mawasiliano katika kujuza uchumi wa buluu," alisema Mohamed.

Aidha, Kaimu Mtendaji Mkuu wa Yas Tanzania, Jerome Albou, alisema mabadiliko ya jina imetokana na kampuni ya Tigo kununuliwa na kampuni ya Hona.

Alisema mabadiliko hayo ya jina hayataathiri utendaji kazi wa kampuni hiyo ambapo pia kwa sasa huduma ya tigo pesa itajulikana kama 'Mixx by Yas'.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mixx by Yas (zamani Tigopesa), Angelica Pesha, alisema huduma hiyo itaendelea kama kawaida na kuchochea matumizi huduma za kifedha kwa njia ya mtandao.

## HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa kwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile.  Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosababisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.



**Mtunzi Adam Fungamwango (0716 350534)**

# Damu ya Mariamu-**41**




"Ushahidi wa meseji, simu za mkononi na klipu mbalimbali zilizokuwa kwenye flashi, zinaonyesha kuwa Materu alikuwa akimpenda sana Mariamu. Msichana huyo mrembo alikuwa na mchumba wa mfanyakazi wake Kamal. Materu alimpa ubosi wa kusimamia gereji kwa makusudi, ili kumuweka karibu na kumpata Mariamu. Alitongoza sana Mariamu, lakini msichana alikataa katakata. Alimuahidi zawadi mbalimbali, ikiwemo kumnunulia gari la kifahari na kumuahidi kumfungulia miradi mbalimbali, lakini alikataa.

Kilichofanyika baada ya hapo, ni kwamba Materu alimtisha Kamal kwa kutumia namba mbalimbali ambazo si za kwake, akitakiwa kumuacha mwanamke huyo la sivyo angeuawa.

Baada ya Kamal kumuambia mpenzi wake, Mariamu alikuwa muungawa, hakumwambia ni nani aliyefanya hivyo ingawa alimjua. Akapoza tu mpenzi wake, lakini akamwambia asiwe na wasiwasi hakuna wa kumuua.

Mariamu alichofanya ni kwenda kumwambia laivu Materu kuwa asidhani kumuua Kamal ndiye itakuwa tiketi ya kumpata. Badala yake akamthibitishia kuwa siku akisikia Kamal ameuawa na yeye atajiua, sasa sijui atakuwa amepata faida gani, kwa sababu hatompata. Ingawa hakusema kitu, lakini hili lilimkera Materu na moyoni akaahidi kumuonyesha. Na alichoamua ni kumuua tu, ili roho yake isiendelee kusononeka kumkosa Mariamu, msichana mrembo alikuwa mikononi kwa mfanyakazi wake, Kamal.

Klipu ambayo mipango hiyo inafanya tumeipata yote na imethibtishwa hapa mahakamani. Baada ya hapo mipango mingine ikafanywa kwa ajili ya kutekeleza maagizo. Wakafanya uchunguzi kuwa Mariam ana tabia ya kutoka nyumbani wake saa moja usiku kupitia maduka yake ya vipodozi. Vijana wawili akatumwa na kuitelekeza kazi ya kumpiga na kitu kizito kichwani kama mmoja wa mashahidi alioona alivyotuambia hapa, akachulikuwa na kupelekwa kwa mhusika mkuu Materu. Baada ya kuthibitisha kuwa ameshakufa, walimnunulia 'trakisuti', kwa lengo la kuupotosha umma kwamba alianguka kwa ugonjwa wa moyo wakati akifanya mazoezi ya kukimbia asubuhi,"Jaji Ken Mahundi alinyamaza kidogo, akanyanyua glasi ya maji iliyokuwa mbele yake akanywa. Halafu akaendelea. "Uchunguzi wao ulibaini kuwa marehemu alikuwa na tabia ya kuamka asubuhi siku za Jumamosi na Jumapili kwa ajili ya kufanya mazoezi ya kukimbia, na kama tunavyoona hata hata siku walioamua kummuua ilikuwa ni Ijumaa, ili kila mmoja aamini kuwa ni kweli alikufa kwa mshtuko wa moyo, kwani maiti ilikutwa Jumamosi, siku ambazo hufaya hivyo.

Ushahidi unaonyesha kuwa Materu alimwaga pesa kwa baadhi ya madaktari kwa ajili ya kupindisha ukweli, badala ya ripoti kusema alipigwa na kitu kizito kichwani, wakasema alianguka wakati akikimbia. Nguvu ya umma ndiyo iliyolazimisha uchunguzi urudiwe, shahidi dokta Shija ametuambia hapa yeye ni mmoja wa madaktari waliofanya ripoti ya pili, wakabaini kuwa alipigwa na kitu kizito kichwani, na hii imethibitishwa na shahidi mmoja hapa aliyeona tukio." Kila mmoja ndani alionekana kupigwa na butwaa na kuvutwa na mtiririko wa kesi hiyo, pamoja na hukumu yake ilivyokuwa inasomwa.

"Baada ya kuona mambo sasa umekuwa mbaya na wanaweza kugundulika, ndipo pia Materu kwa kutumia pesa zake kuwahonga baadhi ya askari wasiokuwa waaminifu ambao waliwaaminisha wakubwa wao kuwa mchumba wa msichana aliouawa ndiye mtuhumiwa na mauaji, kwani waligombana siku chache kabla ya kifo chake na ilihusu masuala ya mapenzi. Hali hii ililazimu kijana Kamal kuishi kwa kujificha, na wakati akifanya hivyo ndipo alipokutana na dokta Shija ambaye baada ya kugundua hilo, badala ya kuripoti polisi akaamua kumsaidia kwani aliamini kuwa hakufanya tukio hilo, kwa sababu alipata taarifa kutoka kwa madokta wenzake jinsi Materu alivyotembeza pesa kwa madaktari na polisi pia. Dokta Shija alimtambulisha kwa mdogo wake afande Willy, na wote kwa pamoja watatu ndiyo kwa kiasi kikubwa waliingia kazini kusaka ukweli wote. Na kwa ujuzi wa hali ya juu wakiongozwa na afande Willy, wakifanikiwa kukusanya ushahidi wote na kuuleta mahakamani ukiwa haina shaka yoyote." Jaji alikuwa katika hatua za mwisho.

"Baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili, mahakama kwa kauli moja imeridhika na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka, hivyo kuwatia hatiani watuhumiwa wote wanane waliohusika na tukio hilo.

Hukumu ni kama ifuatavyo. Mshtakiwa namba moja, Boniphace Materu, mashtakiwa namba tatu hadi namba nane, wote wanahukumiwa kifungo cha maisha jela kwa kuhusika, kushiriki, kuratibu na kupanga njama za mauaji ya marehemu Mariamu kwa makusudi kwani. Haki ya rufaa ipo kwa siku zisizozidi 30. Mashtakiwa namba mbili yeye anahukumiwa kunyongwa mpaka kufa kwa kosa la kumuua kwa kumpiga kitu kizito kichogoni. Na yeye na haki ya kukata rufaa kabla ya siku 30 kuanzia sasa." Akamaliza Jaji Mahundi.

Mazingira ya mahakama yalibadilika. Kutoka kuwa kimya kana kwamba watu wako kwenye ibada kulisikika makofi, mayowe, vigelegele na shangwe kutoka kwa umati wa watu uliofurika ndani ya nje ya mahakama. Hata hivyo kulikuwa na kundi dogo lililomezwa na watu wengi waliokuwa wakishangilia. Wao waliangua vilio. Walikuwa ni baadhi ya ndugu wa wahukumiwa hao.

**Mazingira ya mahakama yalibadilika. Kutoka kuwa kimya kana kwamba watu wako kwenye ibada kulisikika makofi, mayowe, vigelegele na shangwe kutoka kwa umati wa watu uliofurika ndani ya nje ya mahakama.**

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# KOCHA COASTAL UNION AIBUKIA SINGIDA BLACK

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa zamani wa Coastal Union, David Ouma raia wa Kenya ametangazwa kuwa kocha msaidizi wa Singida Black Stars.

**Klabu hiyo imetoa taarifa hiyo siku chache baada ya kuwatimua makocha Patrick Aussems na msaidizi wake Denis Kitambi kutokana na matokeo mabaya ya timu hiyo.**

"Tunaendelea kuboresha idara yetu ya ufundi kwa kuwongeza kocha David Ouma, raia wa Kenya kuwa msaidizi wa kikosi chetu," ilisema taarifa hiyo.

Singida ilimtimua Aussems, raia wa Ubelgiji kutokana na kile ilichodai ni mwendo usioridhisha katika michezo mitatu mfululizo, licha ya jitihada zote kufanyika kutoka kwa uongozi wa klabu hiyo kuwapatia benchi la ufundi kwa kila wanachohitaji.

Hiyo ilikuja muda mfupi tu baada ya kulazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Tabora United uliochezwa, Novemba 25 mwaka huu, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, ikiwa ni michezo ya tatu mfululizo kucheza bila kupata ushindi.



Kabla ya hapo, tayari timu hiyo ilikuwa imelazimishwa suluhu dhidi ya Coastal Union, Uwanja wa New Amaan Zanzibar, Novemba 2 mwaka huu, na kuchapwa bao 1-0 na Yanga kwenye uwanja huo huo, mjini Zanzibar.

"Ukiangalia timu tunazotoa nazo sare ukazilinganisha na Singida Black Stars, tumezipita kiwango kwa kiasi kikubwa, kwa maana hii timu inaonyesha inaanza dalili za kushuka kiwango, Bodi ya Wakurugenzi ikaona ichukue hatua hizi ambazo ni za mwanzo, huko mbele tutaangalia nini kitaendelea," alisema Ofisa Habari wa Klabu hiyo mara baada ya kumtimua Aussem, kocha wa zamani wa Simba.

Ouma, alikuwa kocha wa kwanza kutimuliwa kwenye timu za Ligi Kuu, kabla ya Coastal Union haijacheza mechi yoyote ya ligi.

Hii ni baada ya kutolewa kwenye mechi ya awali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Bravo do Maquis ya Angola, ikipigwa mabao 3-0 ugenini na suluhu nyumbani, lakini kwa sasa amepewa jukumu la kumsaidia kocha wa Singida Black Stars.

Zipo taarifa kuwa timu hiyo ipo kwenye mazingumzo na kocha zamani wa Yanga, Miguel Gamondi (pichani).





Mwandaaji wa pambano la ngumi la 'Fight for Change', Japhert Mashauri, akiwatambulisha mabondia, Michael Ntebeko (kulia) na Fadhil Shaaban baada ya kupima uzito jana kuelekea kwenye pambano leo litakalofanyika ukumbi wa Pulse, Masaki Dar es Salaam. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

## *Ligi ya Wanawake yapata hat-trick, wanaume bado*

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI tayari Ligi ya Soka Wanawake ikiwa na 'hat-trick' hadi kufikia raundi ya tano, Ligi Kuu ya soka wanaume haina 'hat-trick' yoyote hadi kufikia raundi ya 12.

'Hat-trick' ni mabao matatu yanayofungwa na mchezaji mmoja katika mchezo mmoja.

Straika hatari wa Simba Queens, Jentrix Shikangwa, alifunga mabao matatu wiki hii, akiiongoza timu yake kuiadhibu Get Program mabao 6-2, katika mchezo wa raundi ya tano ya Ligi ya Soka Wanawake.

Mabao mengine ya Simba walifungwa na Asha Djaffar, Asha Mwalala, na Elizabeth Wambui.

Ilikuwa ni 'hat-trick' ya kwanza kwenye Ligi Kuu Wanawake, huku ya wanaume ambayo imeingia kwenye raundi ya 11 ikiwa haina 'hat-trick' yoyote.

Mabao hayo matatu, pia yanamfanya straika huyo raia wa Kenya kuongoza kwenye orodha ya wafungaji, akiwa tayari ana mabao sita, katika michezo mitano ambayo ameichezea timu yake.

Simba Queens imeendelea kuongoza ligi ikiwa na pointi 15 katika michezo mitano iliyocheza, ikuifuatiwa na JKT Queens yenye pointi 13 kwa michezo mitano iliyocheza, Mashujaa Queens ikishika nafasi ya tatu, ikiwa na pointi sita, Yanga Princess ya nne, Bonda Queens ya tano, Fountain Gate ya sota, Get Program ya saba na Ceasiaa Queens ya nane, zote hizo zina pointi sita, Alliance Gilrs ya tisa ikiwa na pointi mbili, Mlandizi Queens ikiburuza mkia na pointi yake moja.

Kumekuwa na ukame wa 'hat-trick' kwenye soka la wanaume, kwani mpaka michezo ya raundi ya 12, hadi mechi za juzi, hakuna mchezaji yoyote aliyeingia kwenye rekodi ya kufunga ya kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kulikuwa na 'hat-trick' saba mpaka kumalizika kwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita, huku Stephane Aziz Ki wa Yanga akifunga mbili.

Wengine waliofunga mabao matatu kwenye mechi moja, ni Feisal Salum na Kipre Junior, wote wa Azam FC, , Waziri Shentembo wa KMC, Jean Baleke wa Simba na Ismai Mgunda wa Ihefu.

## Mlandege hakuna wa kuwazuia kileleni

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA msaidizi wa timu ya Mlandege FC, Sabri Ramadhani amesema hakuna timu itakayowazuia kubaki katika nafasi mbili za juu katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar.

Mlandege ilirudi kileleni mwa msimamo wa Ligi hiyo baada ya kushinda mchezo wake wa 13 dhidi ya Kipanga kwa mabao 3-1 mchezo uliopigwa katika uwanja wa Mau A juzi.

Mlandege sas imefikisha ponti 27 wakati nafasi ya pili ikikaliwa na Mafunzo FC yenye alama 26.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Ramadhani alisema mipangao yao ni kuendelea kuwapo kileleni mwa msimamo wa Ligi kwa kushinda michezo miwili iliyobaki ya kukamilisha mzunguko huu wa kwanza ambapo kila timu itacheza michezo 15.

"Kwa hapa tulipofikia hatuna shaka wala wasiwasi na michezo ijayo ya kumalizia mzunguko, wachezaji wapo vizuri wanajituma hasa kwa kusaka matokeo," alisema.

Aidha, akiuzungumzia mchezo wao dhidi ya Kipanga alisema wapinzani wao walikuwa bora kipindi cha pili na ilifanikiwa kumiliki mipira muda mwingi.

Alisema kipindi cha pili walikuja na mbinu ya kushambulia kwa kuchezea mipira mbinu ambayo haikuwasaidia kupata mabao na wakajikuta wamewafunga bao la tatu katika dakika za mwishoni mwa mchezo.

Alisema licha ya ushindi huo lakini haikuwa mchezo rahisi kwakuwa wamecheza na timu yenye wachezaji wazuri na wazoefu katika ligi.

Hata hivyo, aliwapongeza wachezaji na mashabiki wao kwa hamasa kubwa wanayoionesha pindi timu hiyo inaposhuka uwanjani.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SALAH KIPAUMBELE SAUDIA

WINGA wa Liverpool na Misri, Mohamed Salah, 32, ndiye ndoto ya usajili wa Ligi Kuu ya Saudi Aarabia msimu ujao. ***(Mail)***

### ARAUJO AWANIWA MAN UTD

KLABU ya Manchester United inapanga uhamisho wa pauni milioni 50 ili kuwashinda Chelsea kwa ajili ya kumnunua beki wa kati wa Benfica na Ureno, Tomas Araujo, 22, Januari. ***(Sun)***

### GUEHI AITAKA CHELSEA

MLINZI wa Crystal Palace, Marc Guehi, 24, anatamani kujiunga tena na Chelsea, wakati Newcastle United pia bado wanavutiwa na beki huyo wa kati. ***(TeamTalks)***

### AMORIM KUFUATWA

HATUA ya Arsenal ya kutaka mshambuliaji mpya imepata pigo kwa Viktor Gyokeres, 26, anayetaka kumfuata kocha wa zamani wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim kwenda Manchester Utd. ***(Football.London)***

### ISAK AKOMALIWA ARSENAL

ASENAL ina takriban washambuliaji sita kwenye orodha ya wachezaji inaowalenga, akiwamo mshambuliaji wa Newcastle United na Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 25. ***(Caught Offside)***

### LUIZ AWANIWA MANCHESTER

MANCHESTER City na Manchester United zimepewa fursa ya kumnunua kiungo wa kati wa Brazil, Douglas Luiz, 26, na kiungo wa kati wa Italia na Juventus, Fagioli mwenye umri wa miaka 23. ***(Gazzetta dello Sport)***

### NKUNKU HAUZWI

KOCHA wa Chelsea, Enzo Maresca amekanusha kuwa Christopher Nkunku anauzwa, licha ya fowadi huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 27 kuwa na muda mfupi wa kucheza. ***(Times)***

### ALMIRON KURUHUSIWA

FOWADI wa Paraguay, Miguel Almiron, 30, ataruhusiwa kuondoka Newcastle United Januari. ***(Telegraph)***

### REITZ AFUATILIWA

KLABU ya Manchester City pia inamfuatilia kiungo wa kati wa Borussia Monchengladbach, Rocco Reitz mwenye umri wa miaka 22 juu ya uwezekano wa kuhama Januari. ***(GiveMeSport)***

### KIWIOR AULIZIWA

NAPOLI imeiuliza Arsenal kuhusu upatikanaji wa beki wa Poland, Jakub Kiwior mwenye umri wa miaka 24 kwa mkopo Januari. ***(Gianluca di Marzio, via Metro)***

### FERGUSON NJIA MOJA

KLABU ya Brighton imemfanya mshambuliaji wa Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson, 20, kupatikana kwa mkopo katika dirisha la Januari. ***(Telegraph)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# NISTELROOY ATAJWA KUINOA LEICESTER

**LONDON,** England

ALIYEKUWA Kocha wa muda wa Manchester United, Ruud van Nistelrooy ameibuka kuwa mgombea anayeongoza kuchukua mikoba ya kuinoa Leicester City ambayo haina kocha mkuu kwa sasa, kwa mujibu wa ripoti.

**Van Nistelrooy alijiunga na Erik ten Hag pale United msimu wa joto kabla ya kuchukua mikoba ya kuwanoa Mashetani Wekundu hao baada ya kufukuzwa kwa Mholanzi mwenzake.**

Mshambuliaji huyo wa zamani wa United alishinda mechi tatu kati ya nne alizoiongoza- ikiwamo dhidi ya Leicester.

### ●●● Kupewa mikoba hiyo haraka, huku yeye akiwa anataka...

Steve Cooper alifukuzwa kazi na Leicester Jumapili, miezi mitano tu baada ya kuteuliwa kwake.

Kocha huyo wa zamani wa Nottingham Forest alitatizika kuungana na mashabiki wa wapinzani wake wa wakati mmoja na kuifanya klabu hiyo kufikisha pointi kumi katika mechi 12 za ligi.

Siku ya Jumatano usiku, gazeti la The Telegraph lilitangaza habari kwamba Van Nistelrooy anapewa nafasi ya kuchukua mikoba hiyo iliyoachwa wazi, huku machapisho mbalimbali yakitangaza ujio wake utakuwa wa haraka.

Inabakia kuonekana kama kocha huyo wa Uholanzi, ambaye uzoefu wake pekee wa uongozi wa juu ulikuwa wa miezi 11 katika klabu ya PSV Eindhoven.

Wasaidizi wa Cooper Alan Tate na Steve Rands pia walitimuliwa, na kuiacha timu mikononi mwa kocha wa kikosi cha kwanza Ben Dawson.

Van Nistelrooy alikiri hadharani mara kadhaa kwamba alitaka kusalia kama sehemu ya wakufunzi wa United kufuatia kuteuliwa kwa Ruben Amorim kama kocha mkuu.

Hata hivyo, bosi huyo wa Ureno hakufungua njia zozote za mawasiliano na mtangulizi wake katika kipindi chote cha mpito cha Van Nistelrooy.

# HOJLUND AFICHUA ALICHOELEZWA NA AMORIM



**MANCHESTER,** England

RASMUS Hojlund amefichua alichoambiwa na Ruben Amorim wakati wa mapumziko kabla hajaifungia Man United bao la ushindi wa Ligi ya Europa - na kueleza kwa nini anapenda mfumo wa wachezaji watatu mbele ya bosi huyo mpya.

Man United walibuka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Bod/Glimt Alhamisi usiku.

Amorim alianza vyema soka lake la nyumbani kwa United katika uwanja wa Old Trafford, lakini timu yake ililazimika kutoka nyuma na kuwashinda wapinzani wao wa Norway na kuendelea kupanda kwenye jedwali la Ligi ya Europa.

Hojlund ambaye Amorim alilazimika kushukuru kwa kurejea kwake akiwa ndio namba 9 alifunga mara mbili katika kila kipindi na kuwezesha ushindi huo.

Hojlund alikuwa ameachwa nje ya kikosi cha kwanza cha Amorim cha Ligi Kuu England mwishoni mwa wiki huku Mashetani Wekundu hao wakitoa sare ya 1-1 na Ipswich, na Marcus Rashford alicheza kama namba 9 katika mchezo wa kwanza wa Amorim.

Lakini alichukua nafasi yake kwa mikono yote miwili siku ya Alhamisi, na huenda sasa akaweka mkono wake juu kuanza wikendi hii itakaporejea kwenye mechi ya ligi na United dhidi ya Everton.

Akizungumza na TNT Sports baada ya mchezo huo, Hojlund alitoa maelezo kuhusu mazungumzo yake kipindi cha mapumziko kutoka kwa Amorim, ambaye alimpa ushauri kabla ya kufunga bao lake la pili la mchezo.

"Siku zote mimi hujaribu kukaa ndani ya eneo la yadi 16," fowadi huyo alisema. 'Kona ya haraka na tumefanyia kazi aina hizi za mambo.

"Kocha aliniambia wakati wa mapumziko niendelee kukimbilia kwenye nguzo ya kwanza na tuliona jinsi ilivyokuwa," alisema.

Mshambuliaji huyo ameanza vyema maisha yake ya soka United hadi sasa, akifunga jumla ya mabao 18 katika michezo 56 tangu ajiunge na klabu hiyo kwa pauni milioni 72 msimu wa joto wa 2023.



# FIFA yatoa 11 wanaowania uchezaji bora Dunia 2024

**NYON,** Uswisi

SHIRIKISHO la Soka Duniani, FIFA, limetoa orodha ya wachezaji 11 wanaowania tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Dunia.

Orodha hiyo ya wachezaji kwa upande wa wanaume, miongoni mwa wanaowania tuzo hii ni Rodri kiungo wa Manchester City ambaye ni mshindi wa tuzo ya Ballon D'or 2024.

FIFA imetoa orodha hiyo kwa kuzingatia ubora wa viwango vya uchezaji, mafanikio binafsi na mafanikio ya timu kutoka kwa wachezaji hao kwa kipindi cha kuanzia Agosti 21, 2023 hadi Agosti 10, 2024.

Wachezaji walioorodheshwa kuwania tuzo hii ni pamoja na Jude Bellingham, Dani Carvajal, Kylian Mbappe, Federico Valverde, Vinicius Jr wote wanatoka katika klabu ya Real Madrid ya Hispania.

Wengine ni Erling Haaland kutoka Manchester City na kinda Lamine Yamal wa Barcelona.

Na mchezaji bora wa Dunia mara 8, Lionel Messi pia ameorodheshwa sambamba na mkongwe Toni Kroos ambaye amestaafu kucheza soka na kiungo wa Bayer Leverkusen, Florian Wirtz.

# Rodri adokeza siku ya kurudi dimbani

**MADRID,** Hispania

KIUNGO wa kati wa Manchester City, Rodri amefichua kwamba analenga kurejea kutoka kwenye jeraha lake la goti kabla ya mwisho wa msimu huu.

Mshindi huyo wa Ballon d'Or alipata jeraha baya la goti wakati City ilipotoka sare ya 2-2 na Arsenal Septemba 22 mwaka huu.

Rodri alikuwa tayari amekosa wiki kadhaa za kwanza za kampeni kutokana na jeraha la misuli ya paja alilopata wakati wa fainali ya Euro 2024 ya Hispania ilipoifunga England.

Kikosi cha Pep Guardiola kimekuwa na wakati mgumu kutokana na kukosekana kwa kiungo huyo, na kujikuta wakipoteza mechi tano mfululizo.

Katika habari njema zaidi kwa mashabiki wa mabingwa hao wa Ligi Kuu England, Rodri ana matumaini kuhusu kupona kwake.

"Lengo langu ni kurejea msimu huu," alisema mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania akiiambia podikasti ya Gary Lineker ya The Rest is Football.

"Nadhani kwa mtazamo wangu itakuwa chanya kwangu kutokata tamaa.

"Sitaki kufanya makosa. Sijui ni lini. Lengo langu ni miezi sita, saba, lakini utimamu wa mwili utaamua."

Baada ya siku kadhaa za uvumi, Guardiola alifichua kwamba City wangemkosa Rodri kwa kipindi kizima cha kampeni mwishoni mwa Septemba.

"Msimu ujao atakuwa hapa. Msimu huu umekwisha kwake]. Ndivyo ilivyo," alisema kocha huyo kutoka Katalunya.



## Yanga kurejesha furaha

INATOKA UKURASA 24

itakuwa mechi ngumu kwa sababu wametoka kupoteza kwenye michezo yao iliyopita, lakini tumejiandaa kushinda mchezo.

"Kingine ni kwamba hatuendi kucheza na mwalimu mgeni, tunakwenda kucheza na Yanga ambao ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu, kwa hiyo tumejiandaa kucheza na timu siyo kocha mpya," alisema.

Yanga ipo nafasi ya tatu ya msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 24, kwa mechi 10 ilizocheza, huku Namungo ikikamata nafasi ya 13 ya msimamo, ikiwa na pointi tisa kwa michezo 11 iliyocheza.

## Ahoua afichua siri ya penalti

INATOKA UKURASA 24

alisema mchezaji huyo.

Kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, mchezaji huyo amefunga penalti zote mbili ambazo amepewa kupiga kati ya nne ambazo Simba imezipata.

Alipachika mkwaju wa penalti katika mchezo ambao timu hiyo ilicheza dhidi ya Dodoma Jiji na kuiwezesha kushinda bao 1-0, pia dhidi ya KMC, akiiongoza Simba kushinda mabao 4-0, huku mbili zingine ilizozipata zikipigwa na Leonel Ateba, naye pia akiweka zote kwenye kamba, kwenye mchezo dhidi ya Coastal Union ilipotoka sare ya mabao 2-2, na dhidi ya Pamba iliposhinda bao 1-0.

Ahoua alikiri kuwa mchezo dhidi ya Bravo do Maquis ulikuwa mgumu, lakini anashukuru kupata ushindi ambao umepatikana kwa bao alilofunga.

Naye Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema wamefurahishwa na ushindi huo ambao umewapa pointi tatu, huku ikisema michuano hiyo inahitaji zaidi matokeo ya ushindi kuliko maonesho.

"Tumefurahi na ushindi tulioupata kwa kuiheshimisha nchi, hii ni michuano ya Afrika, tunachohitaji ni kukusanya pointi tatu kwa maana hiyo tumetimiza malengo, mashindano haya hayahitaji mbwembwe.

"Kuna wengine wanatubeza kuwa tumepata bao la penalti, lakini wakumbuke kuwa hata kufunga kwa penalti nako kunahitaji umahiri na ufundi, ndiyo maana Simba ilipata penalti yake Ahoua akafunga, wenzetu wakapata lakini kipa wetu Moussa Camara akaokoa, hii yote ni kuonesha tuna wachezaji wenye uwezo, ubora na vipaji, siyo kila penalti ikipatikana basi unaweza kufunga," alisema Ahmed.

Desemba 8, Simba itacheza saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Mohamed Hamlaoui dhidi ya CS Constantine ya Algeria katika mchezo wa Kundi A, Kombe la Shirikisho Afrika.

# AZAM YASHINDA MECHI SITA MFULULIZO LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

USHINDI wa Azam FC wa mabao 2-1 ilioupata juzi dhidi ya Singida Black Stars kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara imeifanya kuondoka na pointi tatu katika michezo sita mfululizo, huku Kocha Mkuu wa timu hiyo, Rachid Taoussi akisema kwa sasa timu yake ni imara.

Tangu ilipolazimishwa suluhu dhidi ya Mashujaa FC kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Septemba 29 mwaka huu, Azam ikaanza kupata ushindi mfululizo hadi kufikia michezo sita kwa kuifunga Namungo bao 1-0, ikaishindilia Prisons mabao 2-0, ikaipa kipigo cha mabao 4-1, KenGold, kabla ya kuichapa Yanga bao 1-0, baada ya hapo ikaifunga Kagera Sugar bao 1-0, kabla ya juzi kushinda mabao 2-1, mechi ikichezwa, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

**Katika michezo hiyo, dhidi ya Namungo, Prisons na Yanga ilicheza ugenini, huku dhidi ya KenGold, Kagera Sugar na Singida Black Stars ikiwa nyumbani.**

Azam imecheza michezo saba bila kupoteza, ambapo mara ya mwisho ilifungwa mabao 2-0 dhidi ya Simba, Septemba 26 kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar, baada ya hapo ikatoka suluhu dhidi ya Mashujaa FC na kuanza kushinda mfululizo.

Yalikuwa ni mabao ya Feisal Salum dakika ya 38 na Jhonier Blanco dakika ya 57 yaliyotosha kuwapa ushindi huo, huku Elvis Rupia akiifungia Singida bao la kufutia machozi dakika ya 62.

Kocha Mkuu wa Azam, Taoussi, alisema timu yake kwa sasa imeimarika kwa kutosha, lakini pia aliwatahadharisha wachezaji wake kuwa makini kwani walikuwa wanacheza na moja kati ya timu bora kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Nina furaha sana mimi, wachezaji na mashabiki wetu, kwa sasa Azam imekuwa timu imara, kwani tumeishinda timu nzuri ya Singida Black Stars, niliwaambia wachezaji wangu wawe makini kuanzia mwanzo hadi mwisho wa mchezo, nashukuru tunasonga mbele," alisema kocha huyo.

Ramadhani Nsanzurwimo, Mkurugenzi wa Ufundi wa timu hiyo, ambaye ameachiwa mikoba ya kuifundisha timu hiyo kwa muda baada ya kutimuliwa kwa Patrick Aussems na msaidizi wake Denis Kitambi, amesema wachezaji wake wameonekana kuathirika na tukio hilo.

"Wachezaji wangu walichelewa sana kuingia kwenye mchezo, nadhani mabadiliko ya makocha yameonekana kuwaathiri, bado akili zao ni kama haziamini au hawajakubaliana na hali, lakini kipindi cha pili tulirudi mchezoni na kuwashambulia wapinzani wetu, hii inanipa matumaini kuwa tutafanya vyema mchezo ujao," alisema.

Ushindi huo, umeipandisha Azam hadi nafasi ya pili ya msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi 27 nyuma ya vinara Simba yenye pointi 28, huku Singida ikisalia nafasi ya nne na pointi zake 24.



Wanariadha wa timu ya Mkoa wa Dar es Salaam wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Tabora United penalti za kumwaga Ligi Kuu*

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Tabora United inaongoza kwa kuzawadiwa penalti nyingi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara hadi kufikia raundi ya 12. Timu hiyo imefanikiwa kupata penalti tano mpaka sasa.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Bodi ya Ligi, pamoja za dawati la takwimu la Nipashe, timu inayoshika nafasi ya pili mpaka sasa ni Simba ambayo tayari imeshapata penalti nne hadi kufikia raundi hiyo, nafasi ya tatu inashikwa na Namungo FC.

Timu zilizofanikiwa kupata penalti mbili kila moja mpaka sasa kwenye Ligi Kuu, ni Azam FC, Coastal Union, JKT Tanzania, Prisons na Yanga.

Kwa mujibu wa takwimu zetu ni kwamba katika ya penalti tano ambazo Tabora United imezipata, nne imewekwa kwenye kamba na imekosa moja, huku Simba ikiweka wavuni penalti zote nne ambazo imezipata, wafungaji wake wakiwa ni Leonel Ateba akifunga mbili na Jean Ahoua naye akitupia mbili.

Namungo imefunga penalti moja tu kati ya tatu ambazo imezipata, Azam FC ikifunga penalti zote mbili ambazo zimewekwa kwenye kamba na Feisal Salum, Coastal Union ikipata moja na kukosa moja, hali kadhalika JKT Tanzania, Hassan Dilunga akipata na nyingine kukosa, Prisons ikipata mbili zote zikifungwa na Nurdin Chona na Jumanne El Fadhili na Yanga ambayo imepata moja na kukosa moja, mpigaji wao akiwa ni Stephane Aziz, aliyepata katika mchezo dhidi ya Pamba Jiji, ikishinda mabao 4-0, na alikosa dhidi ya Tabora United, timu yake ikipokea kipigo cha mabao 3-1.

Jumla ya penalti 28 zimepatikana mpaka sasa kwenye Ligi Kuu, 22 zikiwekwa ndani ya nyavu na sita zikikoswa, kati ya hizo nne zikiokolewa na makipa.

Michezo
Jumamosi Novemba 30, 2024
Nipashe



Rodri adokeza siku ya kurudi UKURASA 22




Wachezaji wa Yanga wakijifua. **PICHA:YANGA**

# Yanga kurejesha furaha

**Na Adam Fungamwango**

●●● Ni baada ya kupoteza mechi tatu mfululizo, leo inaivaa Namungo kwao huku kocha...

KOCHA Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic amesema wamejiandaa vyema kwa ajili ya mchezo wa leo, huku akisema wachezaji wake watapambana kwa kila hali kupata ushindi ili kurejesha furaha kwa wanachama na mashabiki wa timu hiyo.

**Leo, Mabingwa Watetezi wa Ligi Kuu, Yanga watashuka kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, Lindi kucheza dhidi ya Namungo, mchezo unaotarajiwa kuanza saa 12:30 jioni.**

Yanga itaingia uwanjani leo ikiwa na kumbukumbu ya kupoteza michezo miwili ya Ligi Kuu, baada ya kufungwa bao 1-0 na Azam Novemba 2, mwaka huu na ikafungwa 3-1 na Tabora United, Novemba 7 mwaka huu, mechi zote zikichezwa, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Pia itaingia uwanjani ikitoka kupoteza mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi, baada ya kufungwa mabao 2-0 na Al Hilal ya Sudan, Jumanne iliyopita, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kocha Ramovic, amesema kila kitu kimekwenda vyema, ila wamejipanga kushinda mchezo wa leo ili kuwarudishia furaha Wanayanga.

"Maandalizi yamekamilika, hii ni mechi muhimu kwetu, kila kitu kinakwenda vizuri, ila nakiri utakuwa mchezo mgumu ila tumejipanga kuondoka na pointi zote tatu.

Hii itakuwa ni mechi yangu ya kwanza nikiwa na Yanga kwenye Ligi Kuu, na ya kwanza pia nikicheza ugenini, lakini hatichezwi kwa ajili yangu, ila kwa ajili ya timu, najua tumepoteza michezo miwili mfululizo ya ligi, lakini hilo haliwezi kutufanya tusipambane na kupata ushindi," alisema kocha huyo.

Hata hivyo, alisema Yanga inawakosa wachezaji Shadrack Boka, Clement Mzize, huku pia kukiwa na hati hati ya kukosekana kwa kipa namba moja, Djigui Diarra.

"Diarra naye yuko kwenye hati hati, itategemea na hali yake itakavyokuwa, hivyo inawezekana akakaa langoni au la," alisema kocha huyo raia wa Ujerumani.

Naye Kocha Mkuu wa Namungo, Juma Mgunda, amesema wataingia uwanjani kwa kuiheshimu Yanga, kwani pamoja na kupoteza mechi zake kwa siku za karibuni, lakini bado ni mabingwa watetezi.

"Ni mechi ambayo tunahitaji matokeo mazuri, tunakwenda kwa tahadhari kwani tunacheza na timu kubwa,

ENDELEA UKURASA 23

## Ahoua afichua siri ya penalti Simba

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Simba, Jean Charles Ahoua, amefichua kuwa yeye ndiye mpigaji penalti namba moja kwenye kikosi hicho ambapo ameshaaminiwa na Kocha Mkuu, Fadlu Davids na wachezaji wenzake.

Ahoua ambaye ni raia wa Ivory Coast aliyesajiliwa na Simba mwanzoni mwa msimu huu akitokea klabu ya Stella Club d'Adjame ya nchini humo, Jumatano iliyopita alifunga bao kwa mkwaju wa penalti katika mchezo wa kwanza wa makundi wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Bravo do Maquis ya Angola na kuipatia timu hiyo ushindi wa bao 1-0.

Alisema kuwa katika muda mfupi tu ambao amekuja kwenye klabu ya Simba, tayari Kocha Fadlu na wachezaji wenzake wamemwamini kwenye upigaji penalti.

"Nashukuru kwa kocha na wenzangu kuniamini kuwa mpigaji penalti namba moja wa timu, wamekuwa na imani sana na mimi, nashukuru Mungu kwa hilo, pia sijawaangusha kwani zote ambazo nimepewa nimekuwa nikifunga na nitaendelea kufanya hivyo zikipatikana zingine kwa sababu najiamini kuwa naweza kufunga,"




ENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002